


# MUHURI WA TATU

 Habari za jioni, wapendwa. Hebu na tusimame sasa kwa muda kidogo tu kwa maombi. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>2</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunaposikia huo—huo wimbo mtamu, tuna—tunafikiria, Bwana, juu ya ninii...ya kwamba wewe uko karibu. Nasi tunaomba ya kwamba utatupokea usiku wa leo, Bwana, kama watoto Wako, ukitusamehe dhambi zetu zote na makosa, na ukitupa baraka zako, kwa kuwa sisi ni watu wahitaji.

<sup>3</sup> Na katika saa hii nzito tunayoishi sasa, nasi tunaona, kila mwaka, inakuwa ni giza zaidi na zaidi, kwa ulimwengu. Na kuja kwa Bwana kunazidi kuwa kwenye matumaini zaidi na zaidi, wakati Yeye anapojifunua katika...katika Neno Lake na katika kujidhihirisha Kwake. Tumekuja tena, usiku wa leo, Bwana, kujaribu kufanya, mkutano huu, na kukuomba utufungulie, Bwana, Muhuri huu wa Tatu wa Kitabu hiki, ili tuweze kuufahamu, kusudi tujue la kufanya na jinsi ya kuishi, na jinsi ya kuwa Wakristo walio bora zaidi.

<sup>4</sup> Naomba, Mungu, ya kwamba utamfanya kila asiye Mkristo ndani hapa, usiku huu, watambue vile wanavyokuhitaji Wewe. Tujalie. Nami na—naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili atatambua ya kwamba hana budi kuishi kwa uaminifu zaidi ya vile alivyoishi siku zilizopita, ili kwamba sote tupate kuwa katika ule umoja wa upendo wa Kikristo na imani.

<sup>5</sup> Jalia ya kwamba kila mgonjwa miongoni mwetu aponywe usiku wa leo, Bwana. Wao wanatambua vile wao wanavyokuhitaji Wewe. Nami naomba, Baba, ya kwamba utabariki kila kitu kinachotendeka ama kusemwa, kwa heshima Yako na utukufu, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

<sup>6</sup> Vema, tena, usiku wa leo, tumekusanyika pamoja tena kwa ajili ya jambo hili, Ju—Jumatano usiku ya juma hili. Nasi tunamtumainia Bwana, usiku wa leo, kwa ajili ya kumwagwa kwi—kwingi kwa baraka Zake juu ya Neno Lake. Na leo nimekuwa nikisoma, kama kawaida ya sikuzote, na kujaribu kufikiri juu ya mambo ambayo yangukuwa yanafaa zaidi kusema, na jambo lenyewe hasa ni, jinsi ya kulisema, na tena kumtegemea Bwana kunipa tafsiri na maana za—za Neno hili lililoandikwa. Nami ninamshukuru Yeye kwa yale aliyotufanyia katika juma zima hili, ya kwamba tunaninii...juu ya kufunguliwa kwa Mihuri hii.

<sup>7</sup> Na, sasa, labda lingekuwa ni jambo zuri iwapo Jumapili asubuhi, kwenye...Unajua, mara nyingi...Hatumaanishi

kueleweka vibaya, lakini, unajua, ninyi... Inakuwa hivyo. Na basi, labda, Jumapili asubuhi, kama wote walio na swali mioyoni mwao kuhusu jambo hilo, wangeliliandika na kuliweka kwenye dawati hili hapa, Jumamosi usiku, na hivyo nione ni kitu gani. Na halafu nitajitahidi kulijibu kwa ajili yenu, Jumapili asubuhi, Bwana akipenda. Nafikiri jambo hilo lingekuwa ni bora zaidi kuliko vile tulivyokuwa tunapanga, kwa sababu wakati mwingine jambo fulani linaeleweka vibaya, unajua. Na hivyo kwa jinsi hiyo nitalipata ninii... Lingekuwa ni jambo bora zaidi ya kwamba ninge—ningelilipata moja kwa moja, unajua. Lingekuwa tu jinsi linavyopaswa kuwa. Kwa kweli, wakati mwingine, sasa...

<sup>8</sup> Mtu fulani alipiga simu leo na kusema, ya kwamba—ya kwamba, akapiga simu akitaka kujua kama ilikuwa ni kweli eti, kwamba, “Wakati ninii—wakati Unyakuo utakapotukia, kungekuwako na mtu mmoja tu Jeffersonville na mtu mmoja New York, na wengine waliosalia katika nchi za ng’ambo.” Kwa hiyo, unaona, jambo fulani linaeleweka tu vibaya. Halafu mtu fulani alisema, ya kwamba, “Jumamosi usiku, kama Bwana akitupa ule Muhuri wa mwisho, basi Yesu atakuwa hapa Jumapili asubuhi.” Unaona? Kwa hiyo ni ninii—ni ninii... Unaona, hu—huninii... Hilo, hilo si kweli. Nawe huninii... Sivyoo.

<sup>9</sup> Hatujui. Kama mtu ye yote anakwambia ya kwamba wao wanajua ni lini atakuja, unajua wao wamekosea, kwanza, kwa sababu hakuna mtu ajuaye jambo hilo. Lakini tunataka kuishi, leo, kama kwamba ilikuwa ni sasa hivi.

<sup>10</sup> Kwa namna fulani nitawageuza kwingine kwa dakika moja, kwa hiyo iweni tayari. Ni—ninaamini Yesu atakuja mnamo, kabla ya, dakika tatu kuanzia sasa hivi, ya wakati Wake. Mnajua hiyo itakuwa ni muda gani? Ni kama miaka thelathini na mitano. Unaona, miaka elfu moja ni siku moja tu, Kwake, unaona.

<sup>11</sup> Kwa hiyo, unapomsikia mtume hapa nyuma akisema, “Wakati umekaribia,” hapa, “wakati umekaribia.” Mtume alisema jambo hilo katika Ufunuo. Unajua huo umekuwa ni muda gani? Hiyo haijakuwa... Hiyo ilikuwa ni jana tu, kwa Mungu, hata hazijafikia siku mbili bado.

<sup>12</sup> Na, unaona, kama ni dakika tatu, chini ya dakika tatu ya Kuja Kwake, unaona, hiyo ingekuwa ni miaka thelathini, hivi, kwetu, ama kitu cha namna hiyo. Pia angalia jinsi, vile dakika tatu zingekuwa Kwake: Yeye tayari anaamka, ili aje. Kwa hiyo sisi, ninyi... wakati mwingine mnaposoma hapa, Yeye anazungumza katika lugha ya Neno, unaona, si katika lugha yetu.

<sup>13</sup> Na halafu kama ningelijua alikuwa anakuja kesho usiku, kesho usiku, kesho ningesoma na kumwomba anipe Ujumbe wa Muhuri wa Nne. Nami ningeshuka nije hapa niuhubiri Huo, hata

hivyo. Unaona? Ni—ninataka kuwa ninafanya kila siku yale tu ambayo ningekuwa nikifanya kama akija. Nami sijui mahali pengine bora zaidi kuliko kukutwa moja kwa moja kazini, unaona, kazini. Kwa hiyo tunaendelea kutenda kazi tu mpaka Yeye atakapokuja.

14 Wakati mwingine wakati tunaposoma tu, na, sasa, iweni waangalifu sana. Na wakati unaposoma, chukueni kanda, zisikilizeni kwa makini sana. Kwa sababu, utalipata kwenye kanda, kwa sababu wamekuwa wakizicheza kanda hizo, na ni nzuri zinasikika vizuri. Kwa hiyo, mtalisikia vizuri zaidi humo.

15 Sasa, kila mtu anampenda Kristo, natumaini, usiku wa leo, na kila mtu anampenda Yeye?

16 Nitawaambieni nini, wakati mwingine, kitu kinachowachanganya watu, mtu yule ambaye amekuja na hakupata sehemu ya ibada ya ibada, mnaona. Ndipo wanaingia na kukusikia ukirejea kule nyuma, unagusia kule nyuma, kitu fulani, ndipo wao wanachukua hayo, yale yaliyosemwa, nao hawakupata ile sehemu ya kwanza. Basi linawachanganya kabisa, unaona, basi. Nao wanafikiri ya kwamba jambo fulani lilisemwa vinginevyo, lakini si—sivyo Hilo lilivyo.

17 Kwa hiyo kama una swali ambalo hulielewi, liandike tu kwenye kipande cha karatasi. Kilete, wakati wo wote kati ya sasa na Jumamosi usiku. Nami nitajaribu, Jumapili asubuhi, kuninii. . . Kama linatatiza kidogo, unasema, “Vema, sijui *hili* lilimaanisha nini hapa. Sikulipata.” Unajua ninalomaanisha. Ndipo nitajaribu kulijibu kwa ajili yako, Jumapili asubuhi, Bwana akipenda.

18 Sasa, usiku wa leo tutasoma tena kutoka kwenye Neno hili tukufu lililobarikiwa, katika sura ya 6. Nasi tunaanza usiku wa leo na Muhuri wa Tatu. Na hiyo ni aya ya 5, aya ya 5 na ya 6.

19 Na kesho usiku tunamalizia wale wapanda farasi wanne; farasi mweupe, na farasi mwekundu, farasi mweusi, na farasi wa kijivujivu.

20 Nami nataka kusema jambo hili. Ya kwamba, kila wakati, hata mpaka asubuhi ya leo, yapata. . . ninaamka alfajiri na mapema, alfajiri sana na kuanza maombi kabla hakujuwa na makelele, na ninaendelea kuomba tu siku nzima. Lakini asubuhi ya leo, alfajiri, Roho Mtakatifu alikuja mahali nilipokuwa. Na wazi wazi tu kama cho chote kile, ni—niliona Muhuri huu mwingine ukifunguka sasa, barabara kabisa. Sasa—sasa—sasa, Yeye ananisikia, ninajua. Nami ninashukuru sana.

21 Sasa, mtakumbuka tu ya kwamba kuna jambo fulani linalotukia. Hilo, na—natumaini mnalikamata, mnaona, mnaona, ya kwamba kuna jambo fulani linalotukia. Ninataka tu kulijaribu kanisa hili wakati mmoja, na kuona kama kweli wangeweza kushika jambo fulani kabla halijatukia dhahiri.

Sasa kumbukeni, kumbukeni yale niliyowaambia. Na, sasa, Bwana atusaidie.

22 Sasa katika aya ya 5.

*Na alipoifungua muhuri ya tatu, nikamsikia yule wa tatu mwenye uhai akisema, Njoo. . . uone! Nikaona, na tazama, farasi mweusi, na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake.*

*Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru mafuta wala divai.*

23 Sasa hebu na tuwekee msingi jambo hili kidogo tu, na kwenye ile Mihuri tuliyopitia. Kwa sababu, kama vile tu kwenye zile nyakati za kanisa, mbona, tunajaribu kuweka msingi, kuziunganisha kwa namna fulani, mpaka unapoweza. . . Hivyo ndivyo zile nyakati zilivyo hasa kwenye Maandiko, mmoja na huo mwingine, namna hiyo tu. Kama vile kupanda ngazi, na kupanda kipandio, hasa; kimoja kikiingia kwenye kingine, na kurudi namna hiyo, unapopanda kipandio.

24 Na sasa, Mihuri huu, kile. . . Ni Ki—Kitabu cha Ukombozi, kilichotiwa muhuri. Kila mtu anaelewa na jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na Kitabu hiki kimefungwa kwa Mihuri Saba. Ni Kitabu cha mihuri saba. Unaona?

25 Na sasa kumbuka, kama tulivyowaonyesha hilo, na kulichukua kutoka kwa Yereima na wote. Sasa, wao, wakati waliponini. . . Wao waliandika namna *hii*, kwenye kipande cha—cha hati ya mkono, ama karatasi, hasa; ama, si karatasi, bali ilikuwa ni ngozi. [Ndugu Branham anaonyesha mfano wa kukunja na kutia muhuri hati ya kukunjwa, akitumia makaratsi.] Nao wakakunja, namna *hii*. Sasa ile. . . Na halafu mwisho wake uliachwa namna *hiyo*; hiyo inaonyesha ni kitu gani kiko mle. Ndipo inayofuata inachukua mahali pa namna ile ile, inakunjwa namna ile ile, inakunjwa namna *hiyo*. Na halafu, mwishoni hapa, inapasuliwa namna *hiyo*, na mwingine kuachwa.

26 Vema, hicho kilikuwa ni kile Kitabu cha mihuri saba. Sasa hatukuwa tuna Vitabu vya aina *hii* mpaka hivi karibuni. Vitabu zamani vilikuwa ni hati kukunjwa. Vilikunjwa. Na basi wakati wanapotaka somo ama cho chote kile. . . Kwa mfano kama—kama Biblia ilikuwa imekunjwa, unataka kusoma Kitabu cha Isaya; ungefungua hapa kwenye Isaya, halafu uikunjue namna *hiyo*, na kuisoma. Na hiki ni Kitabu cha Ukombozi kilichotiwa mihuri saba.

27 Na sasa tunaona ya kwamba Mwana-Kondoo anatoka, anakichukua Kitabu kutoka katika mkono Wake Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi, na kuivunja ile Mihuri, na—

na kuifungua . . . na kukifungua Hicho, anawafungulia watu ile Mihuri.

28 Na wale Wenye Uhai wanne wanaoketi pale, ambao tuliwachukua katika zile nyakati za kanisa, wale wale Wenye Uhai wanne, unawaona kote kote kwenye Maandiko, nao ndio wanaotangaza kuvunjwa kwa Mihuri hii. Sasa, na tunaona ni Ki—Kitabu cha Ukombozi.

29 Ndipo tulirudi nyuma na tukampata yule—yule Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, na tukamchukua, kuona kazi yake ilikuwa ni nini. Na sasa kwa miaka hii yote, Kristo amekuwa akifanya kazi ya Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu. Sasa, wote wale wanaofahamu hilo, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye amekuwa akifanya kazi ya Mkombozi aliye wa Jamaa wa Karibu.

30 Lakini utakuja wakati kwamba ambapo kazi ya kukomboa itakwisha. Na hapo kazi ya kukomboa itakapokwisha, basi Yeye ataondoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, mahali ambapo ameketi sasa. Lakini hicho si Kiti Chake cha Enzi. “Yeye ashindaye ataketi pamoja nami katika Kiti Changu cha Enzi, kama nilivyoshinda na kuketi katika Kiti cha Enzi cha Baba Yangu.” Hicho si Kiti Chake cha Enzi. Hicho ni cha Roho, Mungu. Kristo, yule Mwana-Kondoo, hicho si Chake. Yeye ni Mungu aliyefanyika mwili, unaona; ambaye ni Mungu yeye yule, aliyefanyika mwili. Sasa, Yeye anaamka kutoka kwenye kiti . . .

31 Kwanza, tangazo lilitolewa, kwa, “Ni nani anayeweza kuja na ku- . . . na achukue Kitabu hiki cha Ukombozi?” Unaona, kwa ajili ya mpango mzima wa ukombozi, tangu Adamu, yote yale aliyopoteza Adamu.

32 Hakukuwa na kitu kilichopotezwa hadi Adamu. Na baada ya Adamu, kila kitu kilikuwa kimepotea, duniani. Na kila kitu kilichoumbwa duniani kilipotea. Na kila kitu kilianguka pamoja na Adamu, kikavuka lile shimo kubwa, ambapo hakuna mtu angaliweza kurudi, hakuna njia kamwe. Mwanadamu, alipofanya dhambi, aliacha njia yake, hakujiachia njia ya kurudi. Na halafu ninii . . .

33 Wakati swali hili lilipoulizwa; Yohana mfunuzi, yule . . . nabii Yohana, alikuwa kwenye lile ono na aliona jambo hilo. Na hapakuwapo na mtu Mbinguni, hakuna mtu duniani, hakuna mtu chini ya nchi, au ye yote yule, alikuwa hata anastahili kukiangalia kile Kitabu. Mnaona? Sasa hebu wazia tu jambo hilo! Ndipo yule Mwana-Kondoo anajitokeza, naye anakitwaa kile Kitabu. Sasa Yohana aliambiwa asilie tena. Yeye alisema, “Tazama, Simba wa Yuda ameshinda, na—na anaweza kukitwaa kile Kitabu na kukifungua.” Kwa hiyo, aligeuka amtafute Simba, naye akaona Mwana-Kondoo. Yule mzee aliita, kasema, “Simba ameshinda.” Lakini alipokuja na kuangalia, ilikuwa ni Mwana-Kondoo akitoka kwenye Kiti cha Enzi.

<sup>34</sup> Sasa, yeye hakuwa ameona jambo Hilo hapo nyuma. Kwa nini? Alikuwa kule nyuma, akifanya kazi Yake ya upatanisho; kwa sababu Yeye alikuwa akitoka damu kwa ajili ya watu, akiwaombea watu, mpaka yule mtu wa mwisho, aliyeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, aingie. Kutakuwa tu na kiasi fulani cha wao kule, na ndio basi. Basi. Hao wengine hata hawatataka kuingia; hawana hamu ya kuingia. Na kwa hiyo, basi, wakati huyo mtu wa mwisho atakapoingia, basi wakati wa ukombozi umekwisha.

<sup>35</sup> Ndipo Mwana-Kondoo anakuja kudai haki Yake ya wale aliowakomboa, na hiyo ni uumbaji wote. Dunia na kila kitu ni mali Yake. Mnaona? Yeye ameikomboa kwa Damu Yake Mwenyewe. Na wakati anapokuja kukichukua Kitabu hiki, kukifungua, mbona, jamani, wao walikuwa . . . Yohana hakulia tena. Ndipo akaangalia, na Mwana-Kondoo huyu alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Alikuwa ameuawa tayari, bali alikuwa hai tena. Na sasa tuliona ya kwamba mwana-kondoo aliyechinjwa ni mwana-kondoo aliyelowa damu, akitoka damu kila mahali. Amechinjwa tayari. Na baada ya kuchinjwa, alifufuka tena. Alikuwa ameketi kwenye Kiti cha Enzi, tuseme, nyuma huko ya Kiti cha Enzi, namna *hii*, akiziombea nafsi zote zile ambazo zingekuja. Ndipo wakati yule wa mwisho alipofika, na ilikwisha, kile . . . Mungu angali alikuwa ameshika kile Kitabu cha Ukombozi. Mnaona? Sasa Yeye anafanya tu kazi ya Jamaa wa Karibu

<sup>36</sup> Kama vile, Boazi alivyoshuka kule, na Ruthu alikuwa tu ameketi pale akingojea hadi Boazi . . . Ninamaanisha, Boazi alikuwa amefanya uko- . . . jamaa wa karibu, kazi ya ukombozi. Mnakumbuka nilipokuwa ninahubiri hayo, si muda mrefu uliopita? Ruthu, kuokota masazo; na, Ruthu, lo lote alilofanya; na kuendelea, na jambo la mwisho lilikuwa, Ruthu, akingojea. Mnakumbuka jinsi nilivyoonyesha mfano wa jambo hilo Kanisani? Huku, Boazi anashuka na kwenda kufanya kazi ya mkombozi aliye jamaa wa karibu. Alifanya jambo hilo; akatoa kiatu chake na kutoa ushuhuda, na kumkomboa Naomi, na, kupitia pale, akampata—akampata Ruthu. Sasa, kwa hiyo, Ruthu alikuwa tu anangojea, kwa sababu alikuwa tayari amefanya kazi. Yeye alikuwa amefanya mambo haya mengine yote, lakini alikuwa anangojea sasa. Na halafu wakati . . . Kanisa linangojea, linapumzika (wengi wao, karibu wote, katika mavumbi ya nchi) wakati Yeye anapofanya kazi Yake ya Mkombozi wa Jamaa.

<sup>37</sup> Sasa ulimwengu ungali unakuwa mbaya zaidi. Na dhambi inalundikana, na—na magonjwa, na shida, na kifo, na huzuni. Wanaume wasiomcha Mungu na wanawake wasiomcha Mungu wanakufa moja kwa moja. Kansa inawala, cho chote kile, wakati

wao hawawezi kuchukua imani ya kutosha huko waliko na kunyosha mkono huko na kuishika.

<sup>38</sup> Sasa angalia. Lakini basi baada ya yote kwisha, baada ya upatani- . . . Uombezi Wake kwisha, Yeye anatokea, anakichukua kile Kitabu kutoka kwenye mkono Wake. Na ndipo Yohana, na kila kitu Mbinguni, na kuanza. . . Zile roho zilizo chini ya madhabahu zinaanza kupiga makelele. Tutapata jambo hilo katika ule Muhuri wa Sita, tena. Na jinsi walivyofurahia! Na— nao wakaanguka kifudifudi, wale wazee, na kumwaga maombi ya watakatifu. Na zile roho chini ya madhabahu zikapaza sauti, “Umestahili Wewe, kwa sababu umetukomboia kwa Mungu, nasi tunarudi duniani kuishi kama wafalme na makuhani.” Loo! kulikuwa na ninii kuu. . .

<sup>39</sup> Ndipo Yohana akasema, “Kila mtu Mbinguni, kila kitu chini ya nchi, na kila kitu,” kilimsikia akimsifu Mungu kuhusu jambo hilo. Hapana budi Yohana aliona jina lake Pale, unajua. Wakati wote huo!

<sup>40</sup> Ndipo aliposema, “Yeye amestahili kukitwaa kile Kitabu cha Ukombozi.” Sasa si mali ya yule Hakimu tena. Ni mali ya Mkombozi, Naye ameisha maliza kazi ya ukombozi.

<sup>41</sup> Sasa anakwenda kulionyesha Kanisa yale aliyokwisha kufanya. Amina. Unaona? Ndipo anachukua tu. . . Lakini kile Kitabu kimefungwa. Hakuna mtu aliyejua, kamwe. Wao wanajua kilikuwa ni Kitabu cha Ukombozi, juu Yake pale, lakini ilibidi kifunuliwe katika siku za mwisho. Kulingana na Ufunuo 10, yule malaika wa saba atapewa Ujumbe wa Hayo. Kwa sababu, ilisema, ya kwamba, “Katika wakati wa kutangazwa kwa wakati wa saba wa kanisa, malaika wa saba, wakati atakapopiga baragumu, siri zote za Mungu zitamalizika, kwa kupiga kwake baragumu.” Halafu, baada ya kufunuliwa Kwake, yule Malaika anashuka kutoka Mbinguni, ambaye alikuwa ni Kristo. Sasa kumbukeni, malaika huyu yuko duniani, mjumbe.

<sup>42</sup> Kristo anashuka, unamwona katika sura ya 10 ya Ufunuo; anaweka mguu mmoja juu ya nchi, na huo mwingine juu ya bahari; upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, macho yake kama. . . na miguu kama moto, na kadhalika; anainua mkono Wake, na kuapa kwa Yeye aishiye milele na milele, kwenye Kiti cha Enzi, ya kwamba, “Hakutakuwa na wakati baada ya haya.” Na hapo anapoapa kiapo hiki, Ngurumo Saba zinatoa sauti zao.

<sup>43</sup> Na yule mwandishi, ambaye, wakati Yohana alipotwaliwa juu, alipaswa kuandika yale aliyoon. Akaanza kuandika. Akasema, “Usiandike Hayo.” Kwa sababu. . . ”Usiandike Hayo.” Hayakuninii. . . Akasema, “Yatie muhuri.” Ndani ya nini? “Yatie muhuri. Usiyaseme.” Unaona, Hayo yatafunuliwa, lakini hata hayajaandikwa katika Neno.

<sup>44</sup> Na wakati alipoanza kufunua ile Mihuri, tunaona ya kwamba, yote ilikuwa ikishangaza. Unaona? Wakati

alipoufungua Muhuri wa Kwanza, yeye alifikiria, “Sasa hapa itasema, ‘Na itakuwa ya kwamba *fulani* atachukua kiti cha enzi, na *fulani* afanye *hivi* na *huyu* atafanya *vile*.’”

<sup>45</sup> Lakini ilipotukia, huyu hapa akatoka akaenda, farasi mweupe, amepandwa, na mpanda farasi juu yake. Vema, “Yeye alikuwa na uta mkononi mwake; naye akapewa taji, baada ya kitambo kidogo,” akasema. Ni hayo tu.

<sup>46</sup> Naye Mwana-Kondoo akageuka nyuma tena, na kuvuta Muhuri mwingine, na hapa akatoka ninii mweusi. . . mpanda farasi mwekundu. “Naye alikuwa na ninii. . . akapewa u—upanga; naye alikuwa anaenda kufanya vita; na akapewa uwezo mkuu, na akaondoa amani duniani, na wakauana.” Hiyo ilikuwa namna ya . . . ingali ni kitu cha siri (sivyo?), wakati alipoufungua.

<sup>47</sup> Halafu inaendelea, na kusema, “Katika siku kabla tu ya hizi Ngurumo Saba, siri zote hapa zinafunuliwa.”

<sup>48</sup> Sasa angalia. Ndipo tunaona, kama ambavyo tumekuwa tukisoma, ya kwamba, katika nyakati zote zilizopita, tumekuwa na watengenezaji, si manabii. Watengenezaji! Na kila huduma inatekeleza kazi ya—yake yenyewe.

<sup>49</sup> Ni kama tu mtu ambaye anafanya kazi ya—ya opareta wa simu, yeye si fundi umeme kabisa. Yeye huenda akafanya kazi ndogo ya umeme. Na kama vile, kama mtu ni mlinda nyaya za umeme, vema, bila shaka yeye. . . Mtu akiwa ni mchimba mashimo ya nguzo za umeme, naye hajafanya kazi yo yote ya ulinzi wa nyaya za umeme, afadhali asizikaribie; lakini huenda akafanya kazi ndogo ya kurekebisha ama jambo fulani lile.

<sup>50</sup> Lakini wakati lile Jambo halisi litakapofunuliwa katika siku ya mwisho, ya sehemu ya mwisho ya Kanisa, ni wakati Mungu amesema ya kwamba Yeye angetutumia, kulingana na Maandiko. Nasi tumeyachunguza kindani kabisa, ya kwamba Yeye alibashiri ya kwamba Roho ya Eliya ingerudi juu ya mtu fulani. Sasa, nafikiri hilo limefanywa dhahiri kabisa. Nasi. . . Nasi tunatarajia jambo hilo kutukia; mahali fulani, mtu aliyetiwa mafuta, katika siku za mwisho, kuinuka. Sasa mtasikia ushupavu mwingi wa dini na cho chote kile, lakini hilo hujaribu tu—hujaribu tu kuninii. . . Ni Ibilisi, akijaribu kuondoa kutoka kwa yule mtu wa kweli yeye atakapokuja, unaona. Lakini atadhihirishwa vizuri. Mnajua vile Eliya alivyokuwa; na angalia jambo hilo, nawe u—utajua. Na halafu wakati yeye. . . Sasa, Wateule watajua.

<sup>51</sup> Si hao wengine; hakika hawatajua. Watalikosa jambo Hilo, maili milioni. Kama. . . Tumepitia hayo yote, na kuonyesha jinsi walivyomkosa Yohana, jinsi walivyomkosa Eliya, jinsi walivyomkosa Yesu, jinsi walivyowakosa katika kila wakati. Nao watafanya jambo lile lile, ‘maana Biblia ilisema watamkosa. Mnaona? Kwa hiyo basi, katika wakati huo, litakuwa ni jambo nyenyekevu sana. Litakuwa rahisi sana. Kwamba lita-. . .



kile kitakachowafanya watu walikimbie. Ni rahisi mno kwao. Tunaona, na daima, wakati watu wanapokuwa werevu na wenye elimu, na kujua mengi sana, ndipo wao wananinii tu. . . Hao ndio wale wanaolikosa, unajua. Unaona?

<sup>52</sup> Yesu hata kidogo hakuchukua watu wa aina hiyo kama (wawe) wanafunzi Wake. Aliwachukua watu wasio na elimu, wavuvi, na hakuna mtu aliyehusika na makanisa yao na kadhalika. Yeye aliwachukua watu wa kawaida tu, watoza ushuru, na wakulima, na wavuvi, na kadhalika, kufanya kazi Yake. Unaona? Maana, wao—wao wanajua wao si kitu, ndipo anaweza kuwafanya wawe kitu fulani, unaona. Mradi tu wanaendelea kujua ya kwamba wao si kitu, basi Mungu anaweza kutenda kazi.

<sup>53</sup> Lakini wakati wanapoanza kufikiri ya kwamba wao wanajua kitu, basi, “Hujui cho chote cha jambo unalopaswa kujua,” Biblia inasema. Na kwa hiyo, basi, tu—tunaona jambo hilo.

<sup>54</sup> Na sasa, tunaona, basi, ya kwamba siri hizi zinapaswa kufunuliwa.

<sup>55</sup> Na kwa nini hawa watu wengine, Wesley, Luther, na wale watengenezaji wakuu, walioleta kuhesabiwa haki, kutakaswa, wakati wa kipentekoste pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu na kadhalika, mbona wao hawakushika Jumbe hi—hizi? Mbona wao hawakuzipata? Ni kwa sababu wao walikuwa ni watengenezaji. Unaona?

<sup>56</sup> Kama kama tu, lichukue upande mwingine, kulikuwako na watu walioingia ambao walikuwa “na nguvu kama wafalme, bali hawakuwa wafalme.” Unaona? Unaona? Huna budi kuangalia lugha ya Biblia ya kitu cho chote. Unaona? Sasa angalia. Lakini, hii, ndiyo sababu kwamba sehemu zote zilizopotea, za ile siri kuhusu kuhesabiwa haki, sehemu ya fumbo juu ya kutakaswa, sehemu ya fumbo kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na, mbona, ni wa aina gani ambao. . . Je! Hawa alikula tofaa, ama alikula komamanga, ama kitu fulani? Unaona? Je! . . . Uzao wa nyoka ulikuwa ni nini? Na—na je! ubatizo ni katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” ama Jina la “Bwana Yesu,” sivyo? Na, loo! mamia ya mambo hayo, yameachwa yakining’inia. Unaona?

<sup>57</sup> Na ndipo katika saa ya mwisho, mtu huyu itabidi aje na kufunua jambo hilo, unaona, ayachukue Maandiko. Litatambulishwa vizuri sana. Angalia. Naam, bwana. Na, sasa, halitakuwa jambo kuu, kubwa mno basi. Linaonekana kama ni kubwa, hapa katika Biblia, litakuwa ni jambo kubwa.

<sup>58</sup> Lilikuwa ni kubwa zaidi namna gani, wakati Yohana alipaswa kushuka kule na kubatiza! Wazia tu sasa. Manabii, kule nyuma, huko nyuma kabisa, Isaya, Malaki, na wote hao walinena habari zake, wakati atakapokuja. Na wakati alipokuja, ni maskini mzee tu, mpweke na asiye na elimu, mwenye masharubu

usoni mwote, na nywele zimejitokeza kama kiwavi kilichojaa manyoya, amevaa ngozi kubwa chakuvu ya kondoo; hana elimu hata, hajaenda shuleni siku moja maishani mwake, tujuavyo sisi. Mnaona? Huyu hapa akaja, ametokea jangwani, hakualikwa hata mara moja mimbarani, naye alisimama kwenye sehemu zile za mto Yordani na kuanza kuwaita watu watubu. Ungeweza kuwazia jambo hilo!

<sup>59</sup> Biblia ilisema, ya kwamba, “Kila kitu kitakuwa kikubwa sana katika siku ile, hata mpaka milima yote itashushwa, na mabonde yote yatajazwa.” Naam, bwana. “Na mahali pote palipoparua patalainishwa.”

<sup>60</sup> Mbona, ninaweza kuwazia nikiwaona kule, nafikiri Yohana angetokea, ama huyu mtangulizi wa heshima wa Kristo, na kuchukua jangwa lote na kulilainisha, na kulipanda nyasi tena. Mnaona? Loo!, wao, nawazia walikuwa wamepanga mambo yote, karibu kama vile walivyofanya leo.

<sup>61</sup> Lakini, lilikuwa ni jambo nyenyekevu sana, hata mitume walilikosa. Wao walisema, “Vema, mbona Maandiko yanasema, kama ninii. . . Unaenda kule ukatolewe sadaka sasa? Kwa nini Maandiko yanasema ya kwamba—ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?”

<sup>62</sup> Yeye akasema, “Yeye amekuja tayari, wala hamkumjua. Na, Mwana wa Adamu, watamfanyia jambo lile lile. Lakini, Yohana,” Yeye akasema, “alifanya yale hasa aliyoandikiwa kutenda. Nao walimtendea sawasawa tu na yale waliyopaswa kumtendea. Na,” kasema, “vivyo hivyo Mwana wa Adamu atateswa.”

<sup>63</sup> Mbona, hakukuwako, nafikiri, theluthi moja ya jamii yote ya Wayahudi waliopata kujua ya kwamba Yesu Kristo alikuwapo duniani. Hawakuninii. . . Huenda walikuwa wamemsikia mshupavu fulani wa dini kule chini mahali fulani, lakini wao hawakumjali, waliendelea tu. “Alikuwa Kwake, na walio Wake hawakumpokea.” Sasa, hapo ndipo ninapoamini hata. . . Sasa, halikusema ya kwamba angekuja kisiri.

<sup>64</sup> Lakini Unyakuo utakuwa ni siri. Kwa hiyo kama ilikuwa ni siri hivyo, Yeye alipokuja, ni zaidi sana jinsi gani Unyakuo hautajulikana! Mnaona? Wao hawatajua jambo hilo. Moja kwa moja watasema, “Vema, nilifikiri tulipaswa kuwa na Unyakuo. Na ni vipi basi mikasa hii yote juu ya nchi?”

<sup>65</sup> Yeye atasema, “Umepita tayari, nanyi hamkujua.” Unaona? Itakuwa hivyo, kama tu mwizi usiku.

<sup>66</sup> Ni kama ki—kitabu nilichosoma, wakati mmoja. Kinaitwa nini? Romeo na Juliet, kilikuwa ndicho hicho, ama kitu fulani? Yeye aliacha, alichukua ngazi akaiegemeza kwenye nyumba, kwa njia fulani. Ninasaha-. . . Ilikuwa ni muda mrefu sana uliopita. Ndipo akaja, akamchukua ninii wake. . . amtwea wakati wa usiku.

67 Sasa, hivyo ndivyo itakavyo—itakavyotukia, na utakuwa uemepita. Si kwamba, watashusha kundi Malaika, wakiwa na sepetu, na kuchimbua makaburi. Biblia ilisema, “Tutabadilishwa, kabla hata hujafumba na kufumbua jicho lako.” Kufumba na kufumbua tu, kila kitu kitakuwa kimekwisha, upesi namna hiyo.

Kusema tu, “Mtu fulani ametoweka.”

68 Vema, nakisia kama tungeweza kuchunguza ulimwengu mzima, leo, kumekuwa na watu mia tano wanaotoweka duniani kila siku, unaona, hawajui kitu juu yake. Wao wanatokea tu, wanatoweka.

Vema, hakutakuwako na wengi sana watakanyakuliwa.

69 Sasa, sitaki kuwashtusha, nami—nami si—si—sidhani ndiyo hivyo, lakini nataka tu kuwaambia yale Yeye aliyosema. Nanyi mnajua hilo, ninyi wenyewe. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji. Watu wanane kutoka ulimwenguni, kuokolewa kwa maji.”

70 Vema, unasema, “Loo, jamani! hakuna haja ya mimi kujaribu.” Hiyo inaonyesha huna aina ile ya imani unayohitaji.

71 Kama kutakuwako tu—kutakuwako na mmoja, huyo atakuwa ni mimi, amina, maana ninaamini. Unaona? Hivyo ndivyo unavyotakiwa uamini, unaona, “Atakuwa ni mimi.” Hakika. Ninataka kuishi karibu sana na Yeye, hivi kwamba nijue Yeye atanichukua wakati atakapokuja. Ninaamini. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kama kuna... Kama watu wengine wasiponyakuliwa, nitakuwapo kwa neema Yake. Maana, Yeye aliniahidi mimi hilo, nami ninajua ya kwamba nita—nitanyakuliwa, maana Yeye hawezi kusema uongo. Nami ninajua nafsi yangu na maisha yangu yanashuhudia, nami ninajaribu kuishi kila siku kama tu kwamba Yeye alikuwa anakuja, kwa hiyo nita—mimi nitakuwa ndiye huyo. Hivyo ndivyo jinsi unavyotaka kujisikia, “Kama kutakuwako na wanane, mimi nitakuwa mmoja wa hao wanane; kukiwa na mia tano, mimi nitakuwa mmoja wa hao mia tano. Sijui habari za jamaa huyo mwingine, lakini mimi ninataka kuwa mmoja wa hao mia tano.” Unaona? Hivyo ndivyo unavyopaswa kushikilia moyoni. Unaona?”

72 Na kama hushikilii hilo moyoni namna hiyo, imani yako ina kasoro. Unaona? Bado huna hakika kwamba umeokolewa, basi. Unakisia tu jambo hilo. Usifanye hivyo. Vema.

73 Hatutauanza Muhuri huu, ama sivyo? Vema. Ninataka, kila usiku... Sijui kama mnajali mimi kuuchukua wakati wenu. Tungeweza kutoka mapema kidogo. Hakuna ninii nyingi sana...

74 Katika kufunuliwa kwa ninihii, kwa Mihuri hii, kumbukeni, kwa kweli ni aya moja tu. Ya kwanza, inanena habari za

kuutangaza, aya ya 2. Karibu vitabu vyote vinavyoelezea, na kadhalika, ukivisoma, ama—ama ukisoma mawazo yao, nami nimeninii—nami daima nimeamini kama karibu wote wanavyofanya, ya kwamba yule mpanda farasi wa kwanza alikuwa—alikuwa ni lile kanisa la mwanzoni. Lakini wakati Roho Mtakatifu alipolifunua hilo, ilikuwa ni kinyume kabisa na jambo hilo. Na kwa hiyo basi, vile ilivyo, ni kuwaonyesheni tu ni kitu gani. Halafu basi ninajaribu . . .

<sup>75</sup> Basi, kwangu mimi, jambo hili ni takatifu sana. Hiyo ndiyo sababu ni afadhali nijibu maswali haya. Na hebu na tulipate, kila mtu akijua moja kwa moja, na kwenye kanda, pia, ya kwamba wao sasa wataelewa. Mnaona? Nilijaribu kuzungumza kwa muda kidogo, usiku, juu ya kuweka msingi, kuwaweka watu . . .

<sup>76</sup> Kuingia haraka na kusukumana, na, hampaswi kufanya hivyo. Mnaona? Lakini, wakati inapotokea, ni ubinadamu. Na kuna joto hu—humu ndani, nanyi—nanyi hamna utulivu.

<sup>77</sup> Lakini mmekuwa waungwana sana, sana. Vizuri mno, katika mkutano huu, kuliko nilivyopata kuona watu wakiwa hivyo, hapa maskanini; na mkiwa mmeketi kwa utulivu, nao akina mama wakiwapeleka watoto wao wachanga kwenye chumba cha watoto wakati walipoanza kulia. Na kila kitu kimekuwa kizuri sana.

<sup>78</sup> Lakini mimi ninajaribu kuweka msingi mpaka ninaposikia tu upako wa Roho juu yangu, kusema Maneno haya, kusema yale yaliyofunuliwa kwangu. Na basi iwapo kwa kufanya jambo hilo, kama nimefanya kosa hapa, mahali fulani, hakika hapa mbele ya watu wote Yeye atanisahihisha kosa hilo. Ni—ninataka jambo hilo. Ni—ni ninii . . . Ninataka Hilo liwe sahihi. Hakuna haja ya kuchukua tu yale unayowazia. Kuna kitu kilicho sahihi, nasi—nasi tunataka Hicho. Tunataka Mungu atupe kile kilicho sahihi.

<sup>79</sup> Kwa hiyo sasa tulimchukua huyu, hawa wapanda farasi, walivyokuwa wakija. Farasi wa kwanza, sasa, nasi tunatambua ya kwamba huyo alikuwa ni yule—yule mpinga-Kristo aliyetoka akaenda zake. Na halafu tunaona, jana usiku, ya kwamba jamaa yule yule aliyetoka akaenda zake kama mpinga-Kristo, kama farasi mweupe, tulimwona akiwa na upanga, jana usiku, amepanda farasi, na kuwaua watu.

<sup>80</sup> Basi, sasa, daima kuna wa maumbile ya kawaida na wa kiroho. Na kwa ajili ya Kanisa, ninataka kufananisha, kabla tu hatujafikia kwenye kule kufunguliwa kwa Muhuri huu.

<sup>81</sup> Ambayo, yale aliyonipa Yeye, nimeyaandika hapa. Nina Maandiko mengi hapa, kurasa saba ama nane za hayo, na ninaporejea.

<sup>82</sup> Angalia, nataka kutoa mfano, wa Kanisa, na niufanye dhahiri sana hivi hamna budi kuuelewa. Mnaona?

<sup>83</sup> Sasa, kulikuwa na bibi-arusi wa kawaida katika bustani ya Edeni. Mnakumbuka jana usiku? Yule bibi-arusi wa kawaida, yeye alikuwa mchumba wa Adamu, akiwa bado hajawa mkewe, maana hakuwa amemjua bado kama mke.

<sup>84</sup> Ni kama tu vile Mariamu alivyokuwa mke wa Yusufu, bali yeye hakuwa amemjua bado. “Alionekana ana mimba.” Unaona?

<sup>85</sup> Sasa, kabla Adamu hajamjua mkewe, yeye alikuwa tu ni bibi-arusi kwake. Vema. Nasi tunaona ya kwamba Mungu. . . Huyu bibi-arusi, alianguka kule katika bustani ya Edeni kwa sababu alishindwa kushikilia Neno la Mungu.

<sup>86</sup> Sasa, Yeye alijua ya kwamba Shetani ataachiliwa kati yao, kwa hiyo akawapa ma—mahali pa kushikilia; kuwakinga. Vema, pale, ni nani angalijua mahali pazuri zaidi pa kukingwa, kuliko Mungu, kama Yeye anajaribu kuwaangalia watoto Wake Mwenyewe?

<sup>87</sup> Kama nikitaka kumwekea ulinzi mtoto wangu Joseph, vema, ndugu, kila kitu. . . Nami nilijua maisha yake yalitegemea jambo hilo, mbona, ningenini. . . nami nilikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Vema, kama ukuta wa futi arobaini wa zege, lenye kuimarishwa kwa chuma, ndio unge-ungeweza kuwa ndicho kitu cha kutimiza jambo hilo, huo. . . Ningeufanya uwe wa futi tisini, ili niwe na hakika, hivyo.

<sup>88</sup> Na kama ninaweza kuwazia jambo hilo juu ya mvulana wangu mdogo, (ambapo, kama uhai wake wa kibinadamu ungeangamia, ninaamini mtoto huyo angeokolewa,) ni zaidi sana vipi, kwa Mungu, kwa mtoto Wake ambaye angepotea Milele! Yeye angemweka nyuma ya nini? Alimweka nyuma ya Neno Lake Mwenyewe. Mradi tu uko kwenye Neno hilo, uko salama. “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni tu mtakalo lote.” Ndio hivyo, Neno.

<sup>89</sup> Kwa hiyo, Hawa alianza kwenda kupunga upepo bustanini, ndipo akakumbana na nyoka, jamaa mwerevu kwelikweli. Naye. . . Naye akaanza. . . Sasa, nyoka alikuwa upande ule mwingine. Mungu anaishi, anakaa, anatenda kazi katika unyenyekevu, kamwe si kwa njia nyingine. Unaona? Sasa, maskini yule mama, mnyenyekevu akiwa anatembea pale, ndipo Shetani akaja kama jamaa mwenye maarifa, mjanja na mwerevu. Naye alitaka kumwuzia utaratibu wake. Mradi tu. . .

<sup>90</sup> Haidhuru Shetani angalimzungukazunguka kiasi gani; mradi tu huyo mwanamke alikaa nyuma ya Neno hili, yeye alikuwa hana shida. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake-Mh.] Mnaona? Kwa hiyo, acha Shetani afanye lo lote atakalo; wewe dumu tu na Neno. Hawezi kufanya jambo lo lote.

Kama akisema, “Mbona, wewe ni mgonjwa.”

“Kwa mapigo Yake nimeponywa.”

“Sawa, utakufa.”

“Yeye atanifufua tena. Aliahidi.”

<sup>91</sup> Unaona, wewe kaa tu nyuma ya Neno. Ni hilo tu. Kristo alienda kwenye usalama wa Neno, Yeye Mwenyewe. “Imeandikwa.” Unaona? Sasa, kaa nyuma ya Neno.

<sup>92</sup> Lakini, Hawa, kwa namna fulani alianza kutoa nafasi, lakini hakuachilia yote. Aliachilia fungu moja tu moja. Na hivyo ndivyo Shetani alivyotaka Yeye afanye. Alimtoa nyuma ya ahadi ya Mungu, kwa kuhoji.

Usijaribu kamwe kuhoji Neno la Mungu. Liamini tu! Unaona?

<sup>93</sup> Kwa hiyo, akatoka Humo. Na kabla Adamu hajawahi kuishi naye, kama mkewe, yeye tayari alikuwa amechafuliwa na Shetani. Naye. . .

<sup>94</sup> Nanyi je! mlipata kuliangalia? Kristo alifanya jambo lile lile, kabisa. Sasa, kwa ajili ya kukomboa, Ilimbidi Mungu awahi pale kwanza. Ulichunguza ukaona habari? Mariamu, kabla hajaja kwa Yusufu, Roho Mtakatifu alikuwa amefika pale tayari. Amina. Unaona? Hapo ndipo Mkombozi alipotokea.

<sup>95</sup> Sasa, sasa angalia, mwanamke wa kawaida alianguka, naye Mungu akafanya njia kwa ajili yake apate kukombolewa. Ingawa alikuwa ameanguka, alifanya njia.

<sup>96</sup> Sasa, huyo alikuwa ni bibi-arusi wa kwanza duniani, alianguka, kabla ya yeye na mumewe hawajafunga ndoa. Bibi-arusi alianguka, kwa—kwa sababu ya—ya hoja, badala ya kudumu na Neno. Alianguka. Naye alianguka akafa, kutengwa Milele. Pamoja naye, akamchukua mumewe na cho chote kile kilichokuwa duniani. Alianguka!

<sup>97</sup> Sasa, lakini, Mungu, akiwa amejaa neema, alifanya njia ya kumkomboa mwanamke huyo. Na sasa Yeye alimwahidi, akimwambia ya kwamba wakati fulani, katika siku zijazo, Neno la kweli litamjia tena. Neno la kweli litafunuliwa Kwake. Sasa kumbuka jambo hilo. Maana, Yeye alimwahidi Kristo, kupitia kwa mwanamke.

<sup>98</sup> Na Kristo ni Neno. Yohana Mtakatifu 1, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili,” mnaona, “na akakaa kwetu.” Mungu aliishi pamoja nasi katika mwili. Yeye alikuwa Neno.

<sup>99</sup> Kabla ya kuwa Neno, ni wazo. Nalo wazo halina budi kuumbwa. Vema. Kwa hiyo, mawazo ya Mungu yakawa uumbaji wakati yaliponenwa, kwa Neno. Hapo ndipo wakati anapoyaleta kwa—kwako kama wazo, wazo Lake, nalo linafunuliwa kwako. Halafu, lingali ni wazo mpaka *wewe* utakapolinena. Hiyo ndiyo sababu. . .

100 Musa aliondoka akaenda zake kuomba. Nguzo hiyo ya Moto ikimzunguka, ndipo Yeye akasema, “Nenda, ukainue fimbo yako kuelekea mashariki, na useme, uite ‘inzi.’”

101 Hakuna inzi. Lakini yeye alienda akainua ile fimbo pale, na akasema, “Na kuwe na inzi.” Hakuna inzi hata kidogo, bado. Akarudi. Lakini yale maneno, wazo la Mungu, tayari limetamkwa. Ni neno, sasa halina budi kutukia.

102 Sasa hamwoni ambapo Yesu alisema? “Ukiuambia mlima huu; si kama nikiuambia. Lakini *wewe* ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka.’”

103 Na jambo la kwanza, nadhani, katika wakati wa Musa, inzi mkubwa wa kijani kibichi akaanza kuvuma. Na, baada ya kitambo kidogo, walikuwa ratili tano kwa yadi. Unaona? Wangetokea wapi? Yeye... Mungu aliwaumba. Hivi hamwoni jinsi... .

104 Mungu anaweza kuuangamiza ulimwengu huu usiku wa leo, kwa—kwa mbu, kama akitaka. Vema, Yeye angeweza kuwalundika mbu mpaka mwezini. Jambo pekee angeweza kufanya ni kusema tu, “Na kuwe na mbu, waja mpaka mwezini.” Hilo lingetosha. Hakuna kemikali ama cho chote kile, wangezidi tu kuongezeka, kuongezeka, kuongezeka. Unaona?

105 Yeye anaweza kufanya atakalo. Yeye ni Mungu, Muumba. Jambo pekee la kufanya ni kilinena tu. [Nugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] Hiyo ni kweli. Yeye ni muumba. Sasa, kama tukipata kutambua jinsi Yeye alivyo mkuu! Unaona? Yeye hufanya tu yale anayotaka kufanya.

106 Yeye anaketi kule na kuwaangalia watu, na maskini waalimu hawa, wakijiona wenye akili, ati, “Hakuna Mungu,” na—na kila kitu. A-ha! Mbona, ni kama tu walivyokuwa Babeli, tena. Babeli, hasa.

107 Sasa tunaona ya kwamba Mungu alimwambia Hawa, ya kwamba, “Baada ya muda mrefu sana, Neno litakurudia.” Sasa, yeye aliangukaje? Nataka darasa langu liliseme. Yeye alianguka kutoka kwenye nini? Hawa alianguka kutoka kwenye nini? Neno. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Neno.”—Mh.] Neno. Ndipo Mungu akasema Yeye angefanya njia ya kumkomboa arudi kwenye Neno tena. Vema. Baada ya muda mrefu sana, Neno lingefunuliwa kwake. Vema. Neno lingekuwa kwa kusudi moja, sasa. Shikilia vizuri sasa, ninayosema. Neno lingemjia kwa kusudi moja, hilo lilikuwa kwa ajili ya ukombozi. Vema.

108 Lakini, mpaka—mpaka wakati huo, yeye alikuwa na kbadala ambacho kinge—ambacho kingefanya kazi mpaka wakati ufike wa lile Neno la asili. Sasa ninyi—ninyi mnaelewa waziwazi? [Kusanyiko, “Amina.”] Unaona? Yeye alimwambia Neno lingemjia tena, lakini, hadi wakati huo, Yeye alimpa kbadala mpaka wakati huo utakapotimia. Kwa hiyo, Yeye alimpa dhabihu ya kutoa, kbadala cha ile Damu.

109 Sasa, ile damu ilikuwa ya mafahali na kondoo, na mbuzi na kadhalika, lakini haikumwondolea dhambi. Unaona? Ilifunika tu dhambi yake. Haikuiondoa, kamwe. Iliifunika. Kwa maana, ilikuwa ni damu ya mnyama, na katika damu ya mnyama kuna uhai wa mnyama. Ilikuwa ni kabadala mpaka iliyo halisi . . . Sasa kaeni sawa.

110 Ile Damu halisi ya binadamu, kama ambavyo wanadamu wangukuwa, ilichukua mwili (Mungu); bila kujuana kimwili, bikira, ule uzazi wa kibikira uliileta hiyo. Sasa Neno la Mungu, ahadi, ikawa Damu, nayo ilifanyika mwili katika utu wa Yesu Kristo aliye Mwokozi. “Damu ya mafahali na mbuzi, na kadhalika . . .”

111 Lakini sasa ngoja. Hapa Mungu aliahidi, akisema jambo hilo litatimia utakapokuja, “Uzao Wake utakiponda kichwa cha nyoka.” Sasa, kama uzao wake ungalikuja tu kama ulivyotoka kwa Adamu, ama kama ulivyotoka kwa nyoka, na kadhalika, basi bado ungalikuwa ni uzao wenye dhambi.

112 Hiyo ndiyo sababu Yohana alilia. Hapakuwapo na mtu, kwa sababu hakuna mtu . . . Kila mtu alikuwa upande wa pili, ule upande wa pili wa handaki, lile shimo refu sana. Lakini unakuja wakati ambapo hiki kabadala cha damu ya mnyama kingeondolewa, wakati ile Damu halisi, iliyofanyika mwili itakapokuja: Mungu, aliyefanyika mwili na Damu. Biblia ilisema Yeye alikuwa hivyo. Timotheo wa Kwanza 3:16, “Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu. Kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili.” Hiyo ni kweli. Kuzaliwa kibikira ndiko kulikotenda jambo hili.

113 Sasa, ile damu ya kondoo na mbuzi ilifunika dhambi, lakini haikuiondoa, kwa maana ilikuwa ni damu ya mnyama. Lakini ilikuwa imekubalika, ilikuwa ni kabadala.

114 Nao kwa kweli wali—walizoea kuwa na kabadala kile, na kwa hiyo waliendelea tu.

115 Na, wakati, Neno halisi lililoahidiwa, lilipodhihirishwa katika Yesu Kristo, ambaye alithibitisha kuwa Mwana wa yule Muumba mkuu, Mungu; naye alithibitishwa, Mwenyewe, kwamba ni Neno lililo hai la Mungu. Whiu! Jamani! Yeye alithibitisha alikuwa ni Hilo. Aliweza kutamka mambo yakawa.

116 Hakuna mwanadamu, ama—ama cho chote ulimwenguni, kingaliweza kufanya jambo hilo. Hakuna kitu duniani kinachoweza kuumba, ila Mungu. Ibilisi hawezi kuumba. Yeye ni mpotoshaji wa kile kilichoumbwa, lakini hawezi kuumba. Dhambi ni haki tu iliyopotoshwa. Unajua ninalomaanisha. Uongo ni nini? Ni kweli iliyonenwa vibaya. Unaona? Uzinzi ni nini? Tendo la kweli la halali lililopotoshwa. Kila kitu katika dhambi, dhambi ni Kweli iliyopotoshwa tu. Sasa, yeye hangeweza kuumba.



117 Lakini wakati Kristo alipokuja, alithibitisha alikuwa ni yule Muumba. Hiyo hapo ile Damu iliyoahidiwa. Sasa ukitaka kusoma jambo hilo, ninii . . . Hebu tufungue tu kwa dakika moja. Tutachukua muda katika jambo hili, hata hivyo, usiku wa leo. Mimi . . .

118 Inanifanya niwe na wasiwasi. Ninafikiria kila mtu anataka kwenda nyumbani, unajua. Na kwa hiyo ni ninii . . . [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Sasa hebu na tufungue Matendo 2. Asante. Nasi tutaninii tu . . .

119 Matendo 2, na tutaona kama hili ni kweli, ama si kweli, kama Yeye alithibitishwa ya kwamba alikuwa Mungu. Vema. Fungueni Matendo 2. Sasa hebu na tufungue hapa kwenye kifungu cha 22, Petro akinena, kwenye Siku ya Pentekoste.

*Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu miongoni mweni kwa miujiza na maajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenye- . . . ni- . . . ninyi wenyewe pia mnavyojua;*

120 “Mtu aliyedhihirishwa, ya kwamba ilikuwa ni Mungu kati yenu.” Kwa mambo yale hasa aliyofanya, akathibitisha ya kwamba ilikuwa ni Mungu. Huyu hapa Petro, akisimama mbele ya Baraza la Wazee, akiwaambia.

121 Nikodemo alijua jambo lile lile. Akasema, “Rabi, sote tunajua ya kwamba Wewe u mwalimu umetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu angeweza kufanya mambo haya asipotoka kwa Mungu.” Mnaona? Wao walijua jambo hilo. Lakini kwa nini?

122 Sasa angalia. Sasa, Hawa aliahidiwa jambo hili. Lakini wakati . . . Huyu bibi-arusi aliposhuka, na akakataa, wakati Neno halisi lilipomjia. Kwa hiyo, huyo mwanamke alikataa kulitambua; yule bibi-arusi wa Kiebrania. Kwa maana, yeye alikuwa ni bibi-arusi wa—wa Mungu; Yeye alimtaliki, katika talaka. Hiyo ni kweli? Yeye alikuwa ni bibi-arusi wa Mungu.

123 Unasema, “Vema, hawakuwa wameishafunga ndoa bado.” Hiyo ni kweli. Lakini Yusufu alimkataa Mariamu kabla . . . Alikuwa akitaka kumwacha Mariamu kabla wao hawajafunga ndoa. Unaona? Yeye alikuwa amemposa.

124 Na wakati alipokuja, Na Neno lile ambalo Yeye aliliahidi, alipokuja kufanya arusi, Yeye alimkuta amejizongazonga kwenye vibadala vyake, vibaya sana, hivi kwamba hangechukua ile ahadi halisi iliyokuwa imeahidiwa, Neno, Kristo.

125 Labda hamlipati. Sasa hebu nilirudie tena. Ninawataka mpate jambo hili, mnaona.

126 Yeye alikuwa ameahidiwa, (bibi-arusi, Hawa), kuwa Mkombozi. Mkombozi wake angekuwa ni Neno. Na wakati

Neno lilipokuja, limefanyika mwili, yeye alilikataa. Alipewa vibadala. Sasa shikilieni jambo hilo, “kibadala.” Alipewa vibadilisho aendelee navyo, mpaka Mkombozi atakapokuja. Na wakati Mkombozi alipokuja, alitaka kuendelea na kibadala chake, na akakataa Neno la kweli. Mnaliona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na huyo alikuwa ni yule bibi-arusi wa Kiebrania.

<sup>127</sup> Hivyo ndivyo alivyofanya Yeye, kwa Hawa wa pili, bibi-arusi, mama wa roho zote za binadamu. Unaona? *Hawa* maana yake ni “mama wa wote,” hao ni wote wa kiro- . . .” wote walio hai.” *Hawa*, “mama wa wote walio hai.”

<sup>128</sup> Sasa, na wakati alipomjia Bibi-arusi wa Kiebrania, yeye alikuwa mama wa wote waliokuwa hai, lakini alilikataa.

<sup>129</sup> Hawa wa kimwili alianguka, huko Edeni, kwa kusikiliza hoja ya Shetani dhidi ya Neno la Mungu. Hivyo ndivyo alivyoanguka. Vema, bwana. Yeye alianguka kwa sababu alifanya hivyo.

<sup>130</sup> Hawa wa kiroho, sasa, huyo ni kanisa, bibi-arusi wa Kristo. Alianguka, si huko Edeni, bali huko Rumi, unaona, kwenye Baraza la Nikea, alipokataa. Kanisa lile la kipentekoste lililoshuka kwenda Nikea, na kusikiliza hoja za Kirumi, badala ya kushikilia Neno, lilianguka. Na kila kitu kilichokuwa mbali naye, kilikufa pamoja naye, karibu naye. Sasa, kama tu vile Hawa wa kimwili alivyoanguka, ndivyo Hawa wa kiroho alivyoanguka. Bibi-arusi wa Mungu alianguka—alianguka kule bustanini. Bibi-arusi wa Kristo alianguka huko Rumi. Unaona?

<sup>131</sup> Angalia, kwa hoja ile ile, dhidi ya Neno la Mungu, yeye pia alizipoteza haki zake za uadilifu, kwa Shetani. Ambapo, tuliona katika kule kuvunjwa kwa Mihuri hii, ya kwamba huyo alikuwa ni Shetani, na angali ni Shetani kule. Biblia ilisema ndio kiti chenyewe cha Shetani. Na kama vile Hawa alivyopoteza haki za—zake za uadilifu, na kuzimpa Shetani, katika bustani ya Edeni; kanisa, bibi-arusi wa Kristo, lilifanya jambo lile lile huko Rumi, wakati walipoipoteza Biblia kuchukua mafundisho yao ya sharti na hoja. Unaona jinsi linavyoonekana kwa mifano? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>132</sup> Wewe fuatilia tu mifano hiyo, huna budi kuja kulipata sahihi. Kama mkono wangu ukionekana kama . . . Kama sijawahi kujiona mwenyewe, na ninaona kivuli changu kikija, nitajua karibu mimi nikoje. Unaona? Lakini, hivyo ndivyo namna ilivyo. Kama ukitaka kuona ni kitu gani kinachokuja, angalia kile kilichokuwako. “Kwa kuwa ninii. . . mambo ya kale yote yalikuwa ni vivuli vya mambo yajayo,” Biblia ilisema. Vema.

<sup>133</sup> Kwa kuwa, yeye alipoteza Neno lake safi, Neno la Mungu, wakati alipoiuza Biblia, na kumweka mtu humo ndani anayesema ya kwamba kanisa lina haki ya kubadilisha lo lote wanalotaka kubadilisha. Nao wamefanya hivyo. Na Bibi-arusi

wa Kristo, bibi-arusi wa kipentekoste, aliua uadilifu wake, kule Nikea, kama tu vile Hawa alivyoza uadilifu wake kwa Shetani katika bustani ya Edeni. Ndivyo ilivyo kabisa. Vema.

<sup>134</sup> Mungu ameahidi; kanisa hili, kanisa hili la kipentekoste, akijua ya kwamba lingefanya hivyo; kama Yeye alivyomfanyia Hawa, Mungu ameahidi.

<sup>135</sup> Kanisa la kipentekoste, je! mnaamini liliuza haki zake za mzaliwa wa kwanza, kabla... uadilifu wake, wakati lilipoondoka pale? Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Hilo, hakika, liliziuza. Basi kanuni ya imani inafaa nini, ambayo msingi wake haumo kwenye Biblia hii? Ninataka mtu fulani atafute kile kinachoitwa Imani ya Mitume, ama hata Neno lake moja tu katika Biblia. Hiyo ni kanuni ya imani ya Kikatoliki, si kanuni ya imani ya mitume.

<sup>136</sup> Soma Matendo 2:38, hiyo ndiyo Imani ya mitume, kama Yeye ana imani yo yote. Naam. Mnaona? Sasa, hiyo ndiyo waliyotumia wakati wote, hata hivyo. Kwa hiyo endapo wewe... Unaona?

<sup>137</sup> Kwa hiyo, wao waliuza haki zao za mzaliwa wa kwanza. Isitoshe, Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, Wapentekoste, hao wengine wote, wamefanya jambo lile lile. Aliunda madhehebu. Rumi, kitu kilichomfanya kufanya jambo hilo, aliunda madhehebu na kumweka mtu fulani awe kiongozi wake. Nao Wamethodisti, Wabatisti, Wapentekoste na kila mmoja, wamefanya jambo lile lile, wakaweka kundi la watu liongoze. Hata Mungu aseme nini, wao... Huna budi kulifanya jinsi wanavyosema lifanywe.

<sup>138</sup> Vema, ni kitu gani? Si kitu cho chote duniani ila ukahaba wa kiroho, mwanamke asiyefaa; naam, bwana, kanuni za imani, kanuni za uongo, za kujitengenezea. Ndipo akawa, wakati alipofanya jambo hilo... Sasa nitathibitisha jambo hili. Akawa kahaba, kwa Mungu. Unaamini Biblia inasema hivyo? Naam, bwana. Binti zake wamefanya jambo lile lile.

<sup>139</sup> Sasa katika Ufunuo 17, kama unataka kuliandika. Yohana alichukuliwa katika Roho, "Na akaona kahaba mkuu ameketi juu ya..." Nasi tulisoma hilo jana usiku. Na kulikuwako na vile vilima saba, na yale hasa aliyoyafanya. Naye aliupa ulimwengu kinyaa cha uasherati wake. Hiyo ni kweli? "Na wafalme wote wa nchi walifanya uzinzi naye," wanadanganya, na kuiba, na kusema uongo, na kulipia toba, na—na maombi ya siku tisa mfululizo, na kila wazimu wo wote ule wa Shetani.

<sup>140</sup> Vema, sasa kumbukeni, alikuwa na mabinti. Vema, kama alikuwa amefanyika mwili, na yuko chini ya utaratibu wa kimadhehebu, basi utaratibu wote mzima ni makosa. Na kama Hawa, kwa kutomtii Mungu, alitupilia kila kitu mautini, ambacho kilikuwa ni cha kwake; na vivyo kila kanisa linalounda madhehebu, hutupilia kila kitu mautini, kinachokitawala. Kweli kabisa. Kitu hicho chote kimeangamia. Hiyo ni kulingana

kabisa na Neno hapa. Soma Ufunuo 17. Na Biblia ilisema ya kwamba Yeye angemteketeza “kwa moto, na watoto wake wote pamoja naye.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kusema, kila utaratibu wa kimadhehebu utateketezwa, pamoja na yule kahaba.

<sup>141</sup> Sasa, hilo halina kupindapinda, na—na ninajua mtaulizwa habari za mambo hayo, na mimi—mimi ninataka kusikia kutokana na jambo hilo. Na mimi ni . . . Hiyo ni kweli, hata hivyo. Biblia ilisema hivyo, kwa hiyo hilo linaifanya sahihi.

<sup>142</sup> Akawa “kahaba.” Unaweza kusoma hilo katika Ufunuo, sura ya 17. Yeye, alifanya nini? Alifanya uzinzi, dhidi ya Mumewe mwenyewe.” “Vema,” unasema, “la, hiyo ni Biblia.” Neno ni Mungu. Na kama ukichukua jambo moja . . .

<sup>143</sup> Hivi ungetaka mke wako ambusu mwanamume mwingine? Kama hakufanya zaidi ya jambo hilo, usingetaka yeye afanye hivyo. Yeye angethibitisha ukosefu wake wa uaminifu.

<sup>144</sup> “Ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake.” Haleluya! Kristo anataka Mke Wake awe msafi kwa Neno. [Ndugu Branham anagongagonga kwenye mimbara mara nne—Mh.] Hivyo ndivyo anavyopaswa kuwa.

<sup>145</sup> Maana, hakuna kitu, hata yodi moja, ama nukta moja, ama chochote, wala yodi, itaondoka katika torati ile, ama kutoka kwenye Kitabu kile, mpaka yote yatakapotimizwa. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita kamwe.”

<sup>146</sup> Usiweke tafsiri yo yote ya kibinafsi Kwake. Yeye anataka Neno lililo safi, lisiloghoshiwa, hata ubembe wo wote usiwepo. Singetaka mke wangu afanye ubembe na mwanamume mwingine. Na unapoanza kusikiliza hoja za namna yo yote, zaidi ya Hilo, unasikiliza, unafanya ubembe na Shetani. Amina! Hilo halikufanyi ujisikie kubarikiwa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu anakutaka ubakie msafi kabisa. Udumu daima hapo na Neno hilo. Dumu Nalo. Vema.

<sup>147</sup> Mungu alimwahidi, kama alivyofanya kwa Hawa katika bustani ya Edeni, kwa Hawa huyu wa mwisho hapa. Ambalo, kanisa la kipentekoste, mwanzo wa kanisa, kanisa lenyewe, ni mama wa watu wote walio hai, kwa sababu, mradi tu wanalihudhuria. Lakini, unaona, wanapochukua dhambi zake, wanakufa pamoja nalo.

<sup>148</sup> Hapa yuaja kijana. Anasema, “Ni—ninataka kumtumikia Mungu.”

<sup>149</sup> Wao wanasema, “Vema, haya ndiyo utakayofanya. Shuka uende pale ukatubu.”

“Vema, nitafanya hivyo. Utukufu kwa Mungu!” Anaenda kule, anatubu.”

150 “Sasa njoo ujiunge nasi.” Haya, haya basi. A-ha. Unaona? Amapatikana. A-ha! Ni kweli, amekufa moja kwa moja pamoja nalo. Unaona? Unaona? Hilo ni ninii tu . . . Hivyo ndivyo Kitabu hiki kinavyofundisha, unaona, si yale ninayosema. Kwa sababu, kinasema Hapa, hivyo. Vema.

151 Sasa, Mungu amemwahidi, kama alivyomwahidi Hawa. Yeye alimwambia Hawa ungekuja wakati ambapo Ne—Neno lingemrudia tena. Sasa mnakumbuka jambo hilo? Kile alichopoteza, kitarudishwa. Maana, kuna Kitu kimoja tu kinachoweza kurudisha, na hicho ni Neno. Hakika.

152 Nimesema, fytua bunduki; usipopiga shabaha, angalia ulipokosea. Huna budi kurudi pale na kuanza tena. Unaona?

153 Na kama ukirudi, unaenda Nikea. Hapo ndipo unapoanza tena, unaona. Rudi, utoke kwenye hayo madhehebu, mbali na kanisa hilo lote. Tumekuwa tukiona Mihuri hii kikamilifu kabisa.

154 Daima nimeshangaa, maishani mwangu mwote, ni kwa nini daima nilizipinga taratibu za madhehebu sana. Si hao watu, la. Hao watu ni kama tu mimi ama wewe, ama mtu mwingine ye yote. Lakini utaratibu huo, utaratibu huo wa kimadhehebu, sasa ninaliona jambo hilo papa hapa. Sikulijua kamwe jambo hilo hadi sasa. Na hiyo ni kweli.

155 Mungu alimwahidi Hawa wa kiroho, yale yale aliyomwahidi Hawa wa kimwili, ya kwamba angerudishiwa Neno tena. Katika siku za mwisho Yeye angelirudishia Kanisa, kwenye Neno la asili tena.

156 Sasa angalia kwa makini sana. Ni—ninataka uwe na hakika sasa. Mungu alimwahidi Hawa, wakati ungekuja ambapo Neno lingerudishwa na Uzao wake. Neno hili, Lenyewe, lingekuwa Mzao. Na wakati wao walipompa kbadala, yeye alikishikilia kbadala hicho. Na wakati Neno lilipomjia, yeye alifanya nini? “Silitaki.” Lilikuwa ni nyenyekevu mno. Halikuonekana ni la kweli, kwake. Halikustaarabika vya kutosha. “Ati zizi la ng’ombe? Loo, jamani! Jamani! Jamaa kama huyo, hajaenda shule hata siku moja? Vema, singeweza kukubali jambo Hilo. Huyu si Masihi. Mtu anayewaachilia watu wengine wampigepige vile watakavyo namna hiyo, halafu uite kitu Hicho ati ni “Masihi”? Anawaacha wamfungue kitambaa usoni, halafu wampige kichwani? Naye eti alijiita ni Nabii, Nabii halisi, aliyetokea?”

157 Kwa kweli, wao hawakuwajua manabii. Yesu alisema hivyo. Alisema, “Kama mngaliwajua manabii, mngalinijua Mimi.” Hiyo ni kweli.

158 Sasa angalia. Lakini wakati Neno lilipomjia, vile, jinsi ile hasa Mungu alivyosema lingekuja; alikuwa ameliwazia namna nyingine. Ninazungunza juu ya bibi-arusi, bibi-arusi wa Kiyahudi, bibi-arusi wa Kiebrania. Huyu alikuwa ni Hawa,

kwanza. Ndipo wakati lilipofika hapa, yeye hakulitaka Hilo. Yeye alitaka kukaa na vibadala vyake.

<sup>159</sup> Sasa, Mungu alimwahidi Hawa wa kiroho, pale Pentekoste, alisema hata kabla halijatendeka, miaka mia nne kabla kanisa halijaanguka kamwe, ya kwamba wao wangeanguka, na wangefanya yale waliyofanya. Lakini, Yeye aliahidi, katika siku za mwisho angelileta Neno tena.

<sup>160</sup> Yesu alisema jambo lile lile wakati alipokuwa duniani; Yeye angelilituma Hilo tena. Na nini . . . Litakuta nini? Litakuta jambo lile lile lililokuta lilipokuja mara ya kwanza. Kweli. Wao wana- . . . Wao, wanataka vibadala vyao. Wanataka madhehebu yao. Wanataka kanuni zao za imani. Wanataka kuishi jinsi tu wanavyotaka kuishi. Nao wanataka, “Vema, mimi ni *Fulani*. Mimi ni wa *Fulani*.” Hakuna kujali yale Mungu anayofanya, kiasi gani Yeye anavyojidhihirisha; angeweza kuwafufua wafu; angeweza kutambua siri za mioyo; angeweza kufanya lo lote ambalo Biblia ilisema Yeye angefanya. Hilo haliwafanyi kitu cho chote. “Kama halihusiani na madhehebu yangu, halina faida.” Unaona?

<sup>161</sup> Jambo lile lile ambalo bibi-arusi wa Kiebrania alilifanya, hiyo ni kweli, unaona, wao walisikiliza kibatala chao. Na Mungu aliwahidi cha kweli. Na Kile kilicho halisi kilipokuja, wao hawakukitaka. Kilikuwa ni kinyenyekevu mno.

<sup>162</sup> Sasa ni jambo lile lile leo, wakati—wakati Jambo Hilo linapojitokeza jukwaani. Sasa, Mungu alisema, katika Malaki 4, ya kwamba Yeye angeleta Mjumbe katika siku za mwisho, ambao ungerejesha. Yoeli alisema, “Nitarudisha miaka yote.” Kila kitu kilicholiwa na Rumi, na kila kitu kilicholiwa na Wamethodisti, na kila kitu kilicholiwa na Wabatisti, kutoka katika lile tawi asilia la kipentekoste, Mungu alisema, “Nitarudisha katika siku ya mwisho.” Hiyo ni kweli.

<sup>163</sup> Naye anaweza kututumia mtu kama huyo atakayekuwa . . . Kitu pekee ambacho Mungu aliwahi kukitumia Neno Lake ni nabii, si watengenezaji; manabii. Wakati wake haukuwa umewadia. Sasa wakati huo unakaribia, na hiyo ndiyo sababu tunalingojea jambo hilo kutukia. Litakuwa jambo nyenyekevu sana na pole sana! Na kwa hiyo . . . Loo, jamani!

<sup>164</sup> Unafikiri hao Wamethodisti matajiri, Wabatisti, na Mpresbiteri, Wapentekoste, watalipokea kamwe?

“Loo!” unasema, “Ati Wapentekoste?”

<sup>165</sup> Wapentekoste ni Walaodikia. “Matajiri, wala hawana haja ya kitu.”

<sup>166</sup> Ilisema, “Hujui kwamba wewe ni maskini.” Huenda mnajenga majengo ya mamilioni ya dola, lakini wewe ungali ni maskini, maskini kiroho.

“Loo!” unasema, “ninafhamu kila kitu.”

“Wewe ni kipofu!”

“Vema,” unasema, “Mungu apewe utukufu, nimefunikwa.”

“Uchi!”

“Vema, nina hakika vijana wetu. Tuna seminari. Sisi . . .”

167 “Nawe hujui.” Sasa hilo ni kinyume chake tu. Sasa, kama Biblia ilisema ya kwamba Kanisa la Laodikia lingekuwa katika hali hiyo . . .

168 Na hakuna mtu duniani angeweza kukana ya kwamba huu sio wakati wa mwisho, kwa sababu, Wakati wa Kanisa la Laodikia, ama, wakati wa saba wa kanisa. Na, tupo hapo sasa, miaka elfu mbili ya pili inamalizia huo. Hakuna nyakati za kanisa tena. Hiyo ndiyo sababu ninyi ndugu wa mvua ya vuli hamngeweza kuanzisha madhehebu mengine. Hakutakuwako na mengine. Hiyo ni kweli. Ni wakati wa mwisho. Amina. Hakuwezi kuwa na nyakati nyingine za kanisa. Zote zimekwisha.

169 Lakini basi kama ujumbe wa kipentekoste ulikuwa ndio ujumbe wa mwisho . . . Ambao, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, zile jumbe tatu za mwisho, zile nyakati tatu za mwisho za kanisa zinafanya Kuzaliwa kukamilifu.

170 Ni kama tu wakati mwanamke anapata, anataka kuzaa mtoto; jambo halisi la kwanza linalotukia ni maji, jambo la pili ni damu, na linalofuata ni uhai.

171 Wakati walipomwua Yesu msalabani, kitu kilichotoka mwilini mwake, kufanyiza ninii mpya . . . kufanyiza Ku—Kuzaliwa. Wao waliuchoma ubavu Wake, Damu na maji vikatoka, na, “Mikononi Mwako ninaiweka Roho Yangu.” Kilichotoka mwilini Mwake ni maji, Damu, Roho.

172 Sasa, Yohana wa Kwanza 5:7 inakwambia juu ya jambo hilo, “Wako watatu washuhudia Mbinguni; Baba, Neno (ambalo ni Kristo,) na Roho Mtakatifu.” Na hawa watatu hupatana katika habari moja; wao si mmoja, lakini hupatana katika habari moja. Na kuna watatu wanaoshuhudia . . . Ama, “Wao ni mmoja,” ninamaanisha. Nimekosea pale. “Na wale watatu wanaoshuhudia duniani, ni maji, Damu, na Roho, nao wanakubaliana katika habari moja.”

173 Unaweza kutakaswa bila ya kuhesabiwa haki. Na unaweza kuhesabiwa haki ya bila kuhesabiwa haki. Unaweza kutakaswa bila ya kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa.

174 Wale wanafunzi, katika Yohana 17:17, walikuwa wametakaswa na kupewa nguvu za kutoa pepo, lakini bado wao hawakuwa na Roho Mtakatifu. Unaona? Kweli. Iliwabidi waendelee hadi wafike Pentekoste, na kungojea mpaka Roho Mtakatifu aje.

175 Hapo ndipo Yuda alipoonyesha rangi zake. Unaona jinsi roho hiyo ilivyojipenyeza kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa? Lakini wakati ilipofikia mwisho, yeye alionyesha rangi zake. Unaona? Hiyo ni kweli.

176 Sasa angalia, sasa, na tupo tumefikia hapa wakati wa mwisho. Na Hawa wa kiroho, kama vile kimwi-...kama vile Hawa wa Kiebrania alivyoahidiwa, bibi-arusi wa Kiebrania aliahidiwa kurudi kwa Neno. Na bibi-arusi wa kiroho kutoka Pentekoste, wakati alipoanguka kule Nikea, basi anaahidiwa katika siku za mwisho kwamba Neno litakuja tena. Sasa mnasema, basi ninii...

177 Mnataka Andiko lingine, chukua hapa, Ufunuo 10. Na ilisema, "Katika ile saa, ule wakati wa ma—malaika wa mwisho, yule malaika wa saba (mjumbe wa saba) atakapoanza kupiga baragumu, siri ya Mungu imekwisha." Unaona? Kule kurudishwa kwenye Neno! Biblia ilisema ya kwamba mjumbe huyu wa siku za mwisho angekuwa wa, "Kuwarudisha kwenye ile Imani asilia tena, wairudie ile Imani ya baba zao." Lakini unafikiri wanalipokea Hilo? La, bwana. "Siku za mwisho, Yeye angelirudisha lile Neno la asilia tena," kama alivyosema katika Malaki 4.

178 Lakini yeye alilipoteza. Sasa, yeye alilipoteza Neno hilo pale Nikea. Hawa alilipoteza kule Edeni; Hawa alilikataa lake pale Kalvari. Nalo kundi la Nikea linalikataa katika siku za mwisho, namna ile ile. Jamani!

179 Lakini wakati Neno lilipokuja katika mwili wa kibinadamu, yeye, Hawa, lile kanisa la Kiebrania, mama wa wote walio hai kiroho, Hilo basi, yeye alilikataa. Alikuwa amekufa sana, katika mapokeo yake na mafundisho ya sharti, hivi kwamba alilikosa Hilo. Vivyo hivyo na huyu, hakika. Vema.

180 Wanapitwa Naye, Neno lililo hai lililodhihirishwa katika mwili, kwa Neno lililoahidiwa. Neno liliahidi kufanya mambo haya. Ahadi ilifanywa, ya kwamba itakuwa hivi katika siku za mwisho. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu." Sasa angalia kile kilichotukia kule Sodoma. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Unaona? Angalia yaliyotukia wakati huo. Unaona? Sasa, Yeye alisema lingekuwa ni jambo lile lile, nasi tunaishi katika siku hiyo. Vema, na ingeweza kuwa, nadhani, ningeweza kupata ahadi zake mia sita kama hizo, kutoka kwenye Maandiko, yanayohusu jambo hilo tu. Mnaona? Sasa, lakini, wao wanalikataa Hilo.

181 Yeye alishikilia mapokeo na kbadala, badala ya lile—lile...Alishikilia damu ya kbadala, badala ya ile Damu halisi. Yesu, lile Neno, alisema, wakati Hilo lilipodhihirishwa kwake, "Kwa sababu yeye alishikilia mapokeo haya..."



Yesu, Neno lililodhihirishwa, alimwambia bibi-arusi, bibi-arusi wa Kiebrania, “Kwa sababu mnashikilia mapokeo yenu, mnalitangua Neno la Mungu kwenu. Haliwezi kuwa na nguvu.”

182 Sasa hiyo ndiyo sababu leo, ya kwamba, ile—ile miamsho tunayopaswa kuwa nayo, tuna miamsho ya kimadhehebu. Hatujawa na uamsho halisi. La, la, la. La, bwana. Msifikiri tuna miamsho. Hatuna. Loo! wao wamepata mamilioni na mamilioni na mamilioni ya wafuasi wa kanisa, lakini hakuna uamsho mahali po pote. La. La.

183 Bi-Bibi arusi hajawa na uamsho bado. Mnaona? Hakujakuwako na uamsho humo, hakujakuwako na madhihirisho ya Mungu kumwamsha Bibi-arusi bado. Mnaona? Tunautarajia huo sasa. Itahitaji hizo Ngurumo Saba zisizojulikana kule nyuma, kumwamsha Yeye tena, unaona. Naam. Yeye atazituma. Aliliahidi. Sasa angalia.

184 Sasa, yeye alikuwa—yeye alikuwa amekufa. Na sasa kama makanisa yangesahau kanuni zao za imani, na kusahau mafundisho yao ya sharti, na kuchukua Biblia tu, wasihi wapewe ahadi, basi itatenda kazi kwao. Lakini, unaona, Yesu alisema, “Ninyi, kwa mapokeo yenu, mnalitangua Neno la Mungu.” Vema, hilo ndilo jambo lile lile leo na Hawa wa kiroho, unaona, yule anayejiita bibi-arusi wa kiroho leo, kanisa. Yeye huchukua Neno la Mungu, naye hatalikubali. Naye anakubali mafundisho ya sharti, badala yake. Kwa hiyo, Neno halina nguvu kwake, unaona, kwa sababu yeye anajaribu kuingiza kanuni zake za imani kwenye Neno, na hilo halitatenda kazi. Sasa, kile tunachohitaji leo. . .

185 Ninaendelea tu kusoma hili hapa, *Mbiu ya Kuja Kwake*, kwenye kichwa vya maneno, “Tunahitaji nabii arudi! Tunahitaji nabii arudi!” Nami nadhani, wakati atakaporudi, hawatajua cho chote juu yake. Ni ninii tu. . . Hiyo ni kweli. Daima imekuwa hivyo, unaona. “Tunahitaji hilo,” kila kitu unachozungumzia, “tunataka nabii arudi, ambaye ataleta Neno la Bwana, asiye na woga. Tunaamini Biblia iliahidi jambo hilo.”

186 Sasa, ninamjua Ndugu—Ndugu Moore na hao wengine, nimekula chakula nyumbani mwake, na cho chote kile, mhariri. Naye ndiye mtu mzuri sana ambaye—ambaye anatembea na viatu vya ngozi, nadhani, mmoja wa jamaa walio bora sana. Lakini, unaona, yeye anajua ya kwamba hatuna budi kuwa na jambo hilo. Na Dada Moore, mmoja wa wanawake walio bora sana, maskini. . . maskini jamaa huyo, nao wanajitolea.

187 Na hilo ndilo moja ya magazeti bora sana yaliyomo hudumani, kwa maoni yangu, ni *Mbiu za Kuja Kwake*. Lakini unaona, wao wanaendelea kutangaza ya kwamba, “Tunataka nabii! Tunataka nabii!” Mnaona? Jamani! Hayo ndiyo wanayozungumzia.

188 Na basi tuko hapa, leo, na kama vile jana na leo, wao wakitangaza kwenye redio, hilo...na makanisa ya Kibatisti na kadhalika, ya kwamba, “Tusiungane na Wakatoliki, lakini hatuna budi kwa namna fulani kushirikiana nao.” Unaona?

189 Na papa hapa, Ujumbe unatoka papa hapa, kuninii, “Kaeni mbali na kitu hicho chenye sumu!” Unaona? Unaona? “Je! watu wawili wanawezaje kutembea pamoja ‘sipokuwa wamepatana?’” Nuru na giza haviwezi kushirikiana pamoja. Nuru inapoingia, giza linaondoka. Unaona? Haiwezi ninii... Ina nguvu kuliko vyote! Huwezi kuizima Nuru, kwa giza. Lakini unaweza kufukuza giza, kwa Nuru. Hiyo ni kweli. Naye ni Nuru, Naye ni Neno. Unaona? Sasa, haya basi, kurudi moja kwa moja. Huwezi kulifanya liseme uongo ama kufanya jambo lo lote baya. Linarudi moja kwa moja mahali hapo tena. Naam, bwana.

190 Ni kama tu vile jamaa fulani wanavyoanza, wanavyojaribu kubishana nawe; kama unajua mahali unaposimama, unajua anavyoamini.

191 Ni kama tu kumchukua sungura na kumwachilia awe huru kwenye zizi, na umeziba kila tundu. Wewe simama tu langoni; lazima arudi. Imekwisha. Unaona? Hana budi kurudi langoni tena, maana hiyo ndiyo njia pekee anayoweza kutokea. Atatokeza kichwa chake apenyeze *hapa*, na karibu avunje shingo yake; halafu aende *kule*, mahali *kule*. Wewe simama tu na umwangelie, naye atarudi moja kwa moja. Unaona? Imekwisha.

192 Hiyo ndiyo njia tu ya kufanya. Dumu na hilo Neno. Unaweza kutangaza kwa nguvu sana kila mahali, kwa kanuni zako za imani, kuvunja tu shingo yako kila mahali, lakini huna budi kurudi moja kwa moja kwenye hili Neno. Unaona? Naam, bwana. Ni lote Hilo.

193 Sasa, unaona, wao—wao—wao—wao hawalitaki Hilo. Hawataki Neno la Mungu. Kwa sababu yeye alishikilia mapokeo yake, alilifanya Neno la Mungu lisiwe na nguvu.

194 Ndivyo ilivyo sasa hivi, kwa Hawa wa kiroho. Yeye hataki... Yeye anataka kubaki na mapokeo yake, na aliache Neno la Mungu. Yeye anashikilia tena madhehebu, na kanuni zao za imani na mapokeo ya wazee wake, badala ya kuchukua Neno la Mungu.

195 Na wakati ahadi ya Neno, katika siku za mwisho, inapoletwa kwake, yeye hataipokea, kwa sababu, ana mapokeo yake, kama alivyokuwa nayo Bibi-arusi wa Kiebrania. Neno halisi, ijapokuwa linadhihirishwa, linahakikishwa, linathibitishwa, yeye hatalipokea. Kwa nini asilipokee? Kwa sababu huyo ndio kivuli chake. Hawezi kulipokea. Hiyo ni kweli. Yeye hawezi kupinga kivuli chake. Unaona? Na imebashiriwa angetenda jambo hilo, kwa hiyo utajizuija na jambo lo lote?

196 Sasa jambo la kufanya tu ni kufurahi kwamba wewe uko ndani. Basi. Kaa ukilingojea. Vema.

197 Mungu aliahidi, katika siku za mwisho, ya kwamba Yeye angedhihirisha na angethibitisha Neno Lake kwake, na hata sasa hangekubaliana na jambo hilo. Yote hayo, Mungu aliyomwahidi, kwa njia ya watumishi Wake, manabii. Mungu aliahidi, kwa njia ya Yesu Kristo. Mungu aliahidi, kupitia kwa Yoeli. Mungu aliahidi, kupitia kwa Paulo. Mungu aliahidi, kupitia kwa Malaki. Yohana. . . Mungu aliahidi, kupitia kwa Yohana mfunuzi, manabii hao wote, vile hasa Ujumbe wa mwisho ungekuwa kwake. Sasa, kama unataka kuandika mambo hayo; bila shaka, nyote mnayajua: Yesu, Yohana 14:12; na Yoeli, Yoeli 2:38; Paulo, Timotheo wa Pili 3; Malaki, mlango wa 4; na Yohana mfunuzi, Ufunuo 10, kumi na saba, moja hadi kumi na saba. Unaona, ni vile vile ambavyo ingetukia sasa! Na, kwa kanisa, ni Kitu gani? Neno lililofanyika mwili likifanywa mwili miongoni mwa watu Wake tena! Unaona? Nao hawaliamini Hilo kamwe.

198 Unajua kile Yesu alichosema wakati Yeye alipoona Yeye. . . wakati alipoitenda hiyo miujiza mbele yao, na kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu? Akathibitisha jambo hilo, alilokuwa anafanya. Alikuwa hivyo. Alikuwa ametimiza kila kitu barabara. Yeye—Yeye aliwaambia, alisema, “Ole wako! Kapernaumu, ambaye umekuzwa hata mbinguni, kama kazi zingali- . . . kazi kuu zingalifanywa katika Sodoma, ambazo zimefanywa kwako, ungalikuwako unasimama hata leo.” Hiyo ni kweli. Na kule Kapernaumu, Yeye hakufanya kitu cho chote ila kuwaponya watu wachache, na kuwaambia siri za mioyo yao, kisha akaondoka. A-ha. Hayo tu. Unaona?

199 Wao hawajui kazi kuu ni nini. Wanafikiria inapaswa kuwa ni mpango mkubwa uliotukuka ambapo kila mtu anasimama, na hakimu anatoa hotuba, na—na bendi zinapigwa, na bendera zinapeperushwa, na ninii—na wanawake waliovalia nadhifu, na ninii zao. . . na kuchezecheza, na wote wenye Ph.D, LL.D., na watu waliovaa kofia kubwa na ndefu, na wenye kosi zilizopinduliwa, na kila kitakataka, kwamba inawabidi wote kuingia. “Hilo ni jambo kuu.”

Mungu anasema, “Huo ni upumbavu.”

200 Naye analeta maskini kitu kidogo ambacho hakijui tofauti kati ya labda ABC, hata kidogo, na kutenda jambo fulani ambalo linaliwasha moto Kanisa halisi. Na hao wengine wanasema, “Kundi la watakatifu wanaojifingirisha.” Mungu anaita *Hilo* “kuu,” na ulimwengu unaliita “upumbavu.” Ulimwengu unaliita *hilo* “kuu,” na Mungu analiita “upumbavu.” Unaona, ni kinyume tu. Unaona? Na jambo ambalo Mungu ameahidi, Mungu atalitekeleza na amelitekeleza. Unaona? Hivyo ndivyo ilivyo.

201 Sasa, hata sasa, yeye angali yuko vile vile alivyokuwa, yule Hawa wa Kiebrania. Yeye hataki tu kutekeleza hilo. Ungeweza kuwafufua wafu; ungeweza kuona Roho wa Mungu. Yesu alishuka, akajithibitisha kuwa Mwana wa Mungu. Kwanza,

Yeye alianza kuhubiri. Vema, wao wakafikiria, “Vema, Mtu wa kipekeepekee. Hivi Yeye ni nani, hata hivyo?” Vema, muda si muda unajua, watu wanaanza kusema . . .

202 Bila shaka, wao walikuwa wamesema, hapo kabla, wakati mtangulizi Wake alipokuja, Yohana, wao walisema, “Wewe ndiwe Masihi?”

203 Akasema, “La. Lakini Yeye anasimama miongoni mweni mahali fulani.” A-ha. Mnaona? Kwa nini? Yeye alijua, wakati ujumbe Wake ulipotangazwa, lile alilipaswa kufanya. Alijua alilokuwa anaenda kufanya.

204 Ni kama tu vile Nuhu alivyokaza kumwangualia Henoko. Wakati Henoko alipoondoka, Nuhu alisema, “Afadhali nikae karibu na safina. Wakati umewadia.” Nuhu alikaza kumwangualia Henoko. Unaona?

205 Naye Yohana aliangualia ishara ambayo Yesu alimwambia, ama Mungu aliyomwambia, aangalie. Alisema, “Yeye anasimama papa hapa hivi sasa, mahali fulani miongoni mweni. Mimi simjui, lakini nitamjua.”

206 Wakiwa wamesimama pale, walisema, “Je! Wewe siye Masihi?” Kasema, “Tumetumwa kutoka makao makuu.” A-ha. Kasema, “Wazee, na wengine wote, walitutuma hapa. Kama wewe ni Masihi, mbona usije na kujijulisha kule, si huku katika kundi hili la kipuuzi hapa! Panda uje kule ukajitangaze.”

207 Yeye akasema, “Mimi si Masihi.” Akasema, “Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani.”

208 Hilo lilipitia juu sana ya vichwa vyao jinsi lilivyoweza kwenda. Wao hawakujua kitu cho chote juu ya hilo, unaona, na hata hivyo wote walikuwa wanamtarajia kuja. “Lakini haingeweza kuwa ni jamaa kama huyo. Loo! jamani! hilo lingekuwa ni jambo baya sana!”

“Umetokea shule gani?”

“Sina.”

“Una kadi yako ya ushirika?”

“Hiyo ni nini?” Unaona?

209 Yeye alitiwa mafuta na Mungu. Akasema, “Kuna jambo moja nililo nalo. Shoka limewekwa kwenye shina la mti.” Sasa, hayo ndiyo tu yeye—hayo ndiyo tu aliyokuwa nayo. Yeye alizungumza lugha ya wakata miti mwituni, si katika lugha ya kasisi; majoka, na mashoka, na miti, na kadhalika. Yeye—yeye hakuzungumza katika lugha ya makasisi.

210 Lakini Yesu alisema hapajatokea nabii kama yeye. “Hapajakuwapo na mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke, kama yeye, hadi siku yake.” Hiyo ni kweli. “Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii.” Alikuwa ni mjumbe wa Agano, alisimama

moja kwa moja katikati ya yale—yale majira mawili ya nyakati, yaliyokuwa yanakuja. Unaona? “Zaidi ya nabii.”

<sup>211</sup> Na kwa hiyo basi—basi wao hawakumjua. Hawakumfahamu. Yeye alikuwa kwa namna fulani mtu asiye wa kawaida, kwa hiyo wakampuuza, unaona.

<sup>212</sup> Ndipo wakati Yesu alipokuja, basi, na hakika wasingempokea Yeye, huyu mvulana wa seremala, hakukuwa na kitu kama hicho, chenye jina baya nyuma Yake, la “mwana haramu.” Na, Yeye, wao wasingenda kumwona jamaa kama huyo.

<sup>213</sup> Lakini, lakini angalia Mungu alilofanya. Yeye aliwachukua wasio na elimu, maskini, wavuvi, wakata miti mwituni, wakulima, na makahaba, na kuwaacha hao waheshimiwa wameketi pale. Kwa nini? Ati nini? Kwa nini Yeye alifanya hivyo? Alifanya jambo kama hilo kwa sababu gani? Ungeweza kuwazia? Kwa sababu kwamba watu hao walimtambua Yeye ni Neno. Sasa hebu na tuwaangalie kwa muda mchache tu.

<sup>214</sup> Hapa pana maskini mzee mvuvi asiyejua cho chote, hawezi kuandika jina lake. Biblia ilisema yeye alikuwa “asiye na elimu na asiye na maarifa.” Analeta samaki wake na kuwaweka pale chini. Anashuka anaenda kule chini kuona kelele hii yote ni ya nini. Lakini kule ndani kabisa ndani yake, alijua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba Masihi. . . Waebrania wote walimtazamia Masihi, kwa sababu kulipaswa kuweko na jambo la Kimaandiko litakapotukia wakati atakapokuja.

<sup>215</sup> Kulikuwako na masihi wengi, walioinuka na kusema, “Mimi Ndiye,” na kuwapoteza, kwa mamia, na—na wakaangamia na kila kitu. Lakini, unaona, hiyo ilikuwa ni kusukumia mbali Yule wa kweli wakati atakapokuja.

<sup>216</sup> Tumekuwa na majoho ya Eliya na mavazi yake, na kila kitu kinginecho, lakini hiyo—hiyo ni—hiyo ni—hiyo ni kusukumia mbali lile jambo lililo halisi wakati atakapokuja. Mnaona? Hiyo ni kweli. Watu wa kila namna ambao wamevaa majoho na mavazi, na wamefunikwa katika kila namna ya shali zilizopinduliwa, na cho chote kile. Hilo halininii. . . Hilo—hilo linathibitisha tu. Ni kama dola ya bandia, inaonyesha kuna nzuri mahali fulani, kama tu unaweza kuipata. Unona?

<sup>217</sup> Kwa hiyo huyu hapa akaja. Sasa hawa waheshimiwa wakatoka, nao walikuwa wameshikilia sana kibadala chao! “Mbona,” wao walisema, “sasa, kama Masihi akija, Yeye bila shaka atakuja kwa Kayafa. Yeye atakuja kwenye madhehebu yetu. Atakuja kwa Mafarisayo.” Masadukayo, “Hivyo ndivyo mnavyodhania! Yeye atakuja kwa Masadukayo.” Na hivyo ndivyo walivyokuwa, unaona, jambo lile lile walilo nalo leo, sasa.

218 Bali Yeye alipokuja, lilikuwa ni jambo la kushangaza. Yeye atakuja, loo! kinyume sana na walilodhania, lakini Yeye alikuja kulingana na Neno. Nao hawakulijua Neno.

219 Hebu niseme jambo hilo, vizuri hasa, ili mninii... litadidimia ndani sana. Ninataka hili lilipatie hasa. Hiyo ndiyo shida yenu leo, mnaona, hamlijui Neno! Mnaona?

220 Yesu alisema, "Mnaweza kuutambua uso wa mbingu, lakini ishara za wakati hamwezi kuzitambua."

Kasema, "Tuna Musa."

221 Kwa hiyo, kasema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi." Hawakumjua Musa, na kwa hiyo hawakujua. Wao walijua tu kanuni fulani ya imani waliyokuwa wamebuni.

222 Sasa hebu na tumchukue huyu mzee mvuvi. Anatua kikapu chake chini. Ana ndevu zake zenye mvi kuzivuta chini, kisha anashuka, "Ninaamini nitaona Yeye ni nani."

223 Ndugu mmoja akasema, "Njoo. Hebu na tushuke twende hapa chini." Kasema, "Huyo ni Jamaa yule yule. Ni Jamaa yule yule waliyesema hivi majuzi. . . Nilikaa Naye usiku kucha jana usiku. Unamjua Yohana, niliyekuwa nikikwambia habari zake?"

224 "Ndio, yule mtu anayeishi mwituni kule chini! Ndio, nilisikia habari zake." "Vema," mzee Simoni, unajua, akasema, "Nilisikia habari zake kule chini. Ndio, alikuwa kule chini, miezi miwili ama mitatu iliyopita, kule chini. Naam."

225 "Vema, akasema. . . Na siku moja alikuwa amesimama pale, akasema jambo la kushangaza. Akasema, 'Unajua, Huyu hapa anakuja sasa hivi!' Wakasema, 'Unajujue?' Akaangalia kule; ni Mtu tu wa kawaida amesimama pale. Akasema, 'Naona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka. Ninasikia sauti ikisema, "Huyu Ndiye. Huyu ni Mwanangu mpendwa Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.'" Ndipo akaingia moja kwa moja majini na akambatiza, kadhalika. Vema, pale, alisema alimjua."

226 "Loo! sijui," Simoni akasema. "Mimi nimesikia yote hayo, mara nyingi." Lakini huyu hapa yuaja. Lakini chini ndani ya moyo wake mlikuwamo na mbegu iliyochaguliwa tangu awali. Unaona? Yesu alisema hivyo. Kweli. Akamwendea. Akaenda pale. Kasema, "Nitashuka niende mkutanoni na nione." Anaenda kule.

227 Yesu alikuwa amesimama pale, Mtu mdogo wa kawaida tu. Akamwendea. Akasema, "Mbona, jina lako ni Simoni. Na jina la baba yako alikuwa anaitwa Yona." Hilo lilimnyenyekeza. Kwa nini? Hiyo mbegu ndogo ya Uzima wa Milele ikagonga mle ndani. Naam, bwana.

228 Kasema, "Ngoja kidogo! Hiyo inakuwaje? Hujapata kuniona. Wala hukumjua baba yangu, maana amekufa miaka mingi. Lakini Wewe hapa unakuja, na kuniambia jambo hilo? Sasa, ninajua ya kwamba Biblia inasema..." Sasa, hiyo

si kurudia yale mzee anayosema. “Lakini Biblia ilisema ya kwamba Masihi atakuwa ni nabii. Huyo hapo. Huyo Ndiye.”

229 Siku moja alipitia Samaria, akishuka kupitia kule pamoja na kundi la Wayahudi. Akawaacha. Na maskini mwanamke huyu mwenye sifa mbaya akatokea, labda ni mama kijana aliye mzuri, unajua. Naye alikuwa amefukuzwa akaenda mitaani, akiwa mtoto. Na Yeye alikuwa anapitia pale. Labda alikuwa akifikiria juu ya jambo fulani. Akaenda pale na kuweka ndoo yake chini. Ndipo akaanza kushusha silingi, mwajua, kuchota maji. Ndipo akamsikia Mwanamume Mmoja akisema, “Nipe maji ninywe.” Akageuka, na pale palikuwa pameketi Myahudi mwenye umri wa makamu hivi.

230 Akasema, “Aisee, Wewe si ni Myahudi? Hupaswi kufanya hivyo. Si desturi kwako Wewe kuzungumza nami. Mimi ni Msamaria.”

231 Akasema, “Lakini kama unajua ni Nani unayesema naye, ungeleta . . . ungeniomba Mimi nikupe maji.”

232 Kasema, “Iko wapi ndoo yako?” Unaona? “Iko wapi kamba yako?”

“Vema,” Yeye akasema, “maji nikupayo ni Uzima.”

233 “Ati nini?” Unaona? “Mbona,” akasema, “mbona, ninyi nyote mnataka kuabudia Yerusalemu. Na baba zenu waliabudia . . .”

234 “Loo!” Akasema, “hiyo ni kweli, lakini,” kasema, “sisi Wayahudi tunajua tunachoabudu. “Lakini,” kasema, “unajua, wakati unakuja ambapo—ambapo watu hawataabudia Yerusalemu ama katika mlima huu.” Akasema, “Wao—wao watamwabudu Mungu katika Roho, kwa maana Yeye ni Roho, Roho na Kweli.” Vema, yeye akaanza kujifunza, unajua.

Naye akasema, “Nenda kamwite mumeo uje naye hapa.”

Akasema, “Ati mume wangu? Sina mume.”

235 “Mbona,” kasema, “hiyo ni kweli.” Kasema, kasema, “Umekuwa ukitembea na watano, na una wa sita sasa.” Kisha akasema, “Umekuwa na watano. Na—na, wewe, wajua. Umesema kweli.”

236 Angalia! Ilikuwa ni nini? Ile Nuru iligusa ile mbegu. Ilikuwa imekaa pale, ambayo ilinenwa na Mungu. Naam, bwana.

237 Ile mbegu ilikuwa duniani. Wakati Mungu alipoyaondoa maji, na jua likaiangazia, ikachipuka. Hiyo ni kweli. Unaona? Hilo tu ndilo ililohitaji, ilihitaji jua. Ilihita tu nuru. Ndio, bwana.

238 Halafu wakati Roho Mtakatifu, ndani Yake, alipoyaondoa maisha yake ya nyuma, na kumwonyesha hayo, ile Nuru iliiangazia. Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Akasema, “Sasa, tunajua, ninajua jambo hilo, ya kwamba Masihi ajapo, hivyo ndivyo atakavyokuwa. Nasi hatujakuwa na

nabii kwa mamia ya miaka. Hatujawahi kuwa na nabii wa kweli, kwa mamia ya miaka.” Ndipo akasema, “Jinsi inashangaza ulivyoniambia juu ya mume wangu, na ukaniambia nimekuwa na wangapi, na kadhalika. Mbona,” kasema, “mimi sielewi na jambo hili.” Kasema, “Masihi ajapo, vema, Yeye atafanya hivyo. Lakini U nani Wewe?”

Yeye akasema, “Mimi Ndiye.”

Hilo lilitosha. Unaona? Malaya!

<sup>239</sup> Nao makuhani waliangalia pande zote na kusema... Vema, hawana budi kujieleza kwa kusanyiko lao. Kasema, “Msijipumbaze na Jamaa yule. Yeye—Yeye amepagawa na pepo. Hivyo tu.” Sasa, hiyo ndiyo tofauti iliyopo. Hilo ndilo jambo lile lile leo. Unaona? Jambo lile lile leo, linatimia barabara. Naam. Naam, bwana.

<sup>240</sup> Yeye, alijua jambo hilo, kwa sababu ile Nuru ilianguzia Hiyo. Wao walininii. . . Hao wavuvi, wakata miti mwituni, wakulima, watoza ushuru, malaya, waliona ndani yake yale Maandiko rahisi yaliyosema Yeye atatenda. Nao Mafarisayo hawangeweza kuona jambo hilo, kwa sababu ya mapokeo yao. [Ndugu Branham anatulia na kuashiria kwa namna fulani. Kusanyiko linaitikia kwa kuthibitisha—Mh.] Hawakuweza kuliona, kwa sababu mapokeo yao. Lakini yule kahaba, wakulima, na hao wengine wote, waliliona Hilo, wale wote waliochaguliwa tangu zamani. Wakati mashaka yalipoondoka, ile mbegu ikaanza kumea. Hiyo ni kweli.

<sup>241</sup> Yeye alifanya nini? Alisema, “Vema, ninafurahi nimekutana na Masihi”? Loo! hapana, ndugu. Moja kwa moja akaingia mjini. Alisahau maji yake. Akasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! haimkini hiki ndicho kitu kile hasa ambacho Maandiko yanasema Masihi atafanya? Je! hili ndilo lile lenyewe?” Nao watu waliweza kuona jambo lile lile.

<sup>242</sup> Kama vile Yesu Kristo alivyosema katika Yohana Mtakatifu 14:12, jambo hilo litatukia tena. Yeye alisema jambo hilo pia katika Luka, wakati aliposema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Jinsi Mungu alivyojidhihirisha katika Mwanadamu, na akatambua ni nani aliyekuwa nyuma Yake; na yale Sara aliyotenda, akicheka hemani. Na Maandiko haya yote, ya Malaki, na kadhalika, yaliyobashiriwa katika siku za mwisho. Waebrania 4 ilisema, wakati “Neno” litakaporudi. Malaki 4 ilisema Hilo lingerudi kwa njia ya mtu. Waebrania 4 ilisema, “Neno la Mungu hu yatambua mawazo yaliyo moyoni.”

<sup>243</sup> Nao wanaweza kuona jambo hilo likifanyika, na kulikataa moja kwa moja. Mapokeo yao hulificha na kulitangua. Vema, tuko tu mahali hapo sasa. Hivyo tu. A-ha.

<sup>244</sup> Unajua, Yeye angeweza kufanya jambo lile lile leo. Angekuja moja kwa moja jukwaani na kufanya mambo yale yale aliyofanya wakati huo, kama tu Yeye alivyosema angefanya. Unaona? Yeye



aliahidi kufanya jambo hilo. Aliahidi kufanya jambo hilo. Na kama Yeye angefanya jambo lile lile, yule mjumbe wa Laodikia anapaswa kulinya.

<sup>245</sup> Na basi kanisa la Laodikia likiona jambo hilo likitendeka, wao watafanya vile vile tu kama lile kanisa la Kiebrania lilivyofanya hapo mwanzo. Haidhuru linathibitishwa vizuri namna gani, loo! wao wangepanya jambo hilo, hata hivyo. Loo! jamani!

<sup>246</sup> Sasa, Hilo linasema ya kwamba lingefanyika. Tungerudi kwenye Neno la asili, na kudhihirishwa kama ilivyoahidiwa, kuirudisha tena Imani, Imani ya asili, tena. Na kama Yeye alijitambulisha kwamba alikuwa anaishi miongoni mwa watu Wake, kwa kufanya mambo haya; Yeye hata angeruhusu picha Yake ipigwe, akalithibitisha kisayansi. Na bado hawaliamini. Na kuthibitishwa, akaruhusu jicho la kimitambo la kamera limpige Yeye picha akiwa amesimama pale, Nguzo ile ile ya Moto, ile ile jana, leo, na hata milele, Waebrania 13:8, kuonyesha kwamba hilo—hilo ni jambo la kisayansi, na kwa kila hali, kisayansi katika ulimwengu wa kiroho. Kwa kila njia hilo lingaliweza kuthibitishwa, limethibitishwa.

<sup>247</sup> Na, unajua, wao labda wangepanya jambo lile lile. Labda wangepiondokea moja kwa moja na kufanya jambo lile lile kama walilofanya.

<sup>248</sup> Ee, Mungu tusaidie! Loo! Tutasimamia hapa tu. Lakini, Mungu tusaidie kuona sasa, ombi langu, tunapokuja sasa. Maana, Sitaki kuwakawisha sana. Mungu tusaidie kuona. Ninaamini labda, Roho akiwa juu yetu, ingekuwa ni sasa hivi ambapo angetusaidia kufunua, kufungua Muhuri huu.

<sup>249</sup> Hebu na tusome. Tunapooni hali lilimo kanisa, tunaona mahali lilipokuwa, tunaona kile walichofanya, tukaona mahali linapopaswa kufikia, tunaliona pale, na tunaona yale waliyopaswa kufanya. Walifanya jambo lilo hilo. Sasa mnaona mahali tulipo? Wewe toa uamuzi. Mimi siwezi kuamua. Mimi ninahusika tu na kuleta Neno hili. Jinsi tu ninavyopewa, ndivyo ninaweza kulitoa. Mpaka nilipewe, siwezi kulitoa; hakuna mtu mwingine awezaye.

*Na alipoifungua muhuri ya tatu, nikamsikia yule wa tatu mwenye uhai akisema, Njoo uone! Nikaona, na tazama, farasi mweusi; na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake.*

*Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, lakini usiyadhuru mafuta wala divai.*

<sup>250</sup> Sasa, yule Mwana-Kondoo anacho kile Kitabu mkononi Mwake, akiivunja ile Mihuri. Amevunja wa kwanza, wa pili, na sasa Yeye anavunja wa tatu. Na anapouvunja, yule Mwana-

Kondoo anauvunja, Muhuri wa Tatu,—yule Mwenye Uhai wa tatu. . .

251 Sasa ni wangapi wanaojua Yule Mwenye Uhai wa tatu alionekana? Alionekana kama mwanadamu. Wa kwanza alionekana kama simba; yule mwingine alionekana kama ndama, ama maksai; na wa tatu alionekana kama mwanadamu, kama mwanadamu. Naye akasikia yule—yule Mwenye uhai, yule—yule Mwenye uhai. Yule Mwenye uhai, kama mwanadamu, alimwambia Yohana, “Njoo, uone ni Kitu gani, siri hii iliyofichwa.” Zamani zote katika ile miaka ya ukombozi, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, imefichwa chini ya Muhuri huu, yale yatakayotukia. Sasa, “Njoo, uone ni Kitu gani.”

252 Na kwa hiyo Yeye anaufungua. Ngurumo inalia, na Mwana-Kondoo anafungua Mihuri.

253 Sasa, na Yohana akaenda, aone ingekuwa ni kitu gani. Yeye aliona nini? Aliona farasi mweusi. Na aliyempanda alikuwa na mizani, ama mizani, mkononi mwake. Sasa, hilo ndilo jambo la kwanza aliloona. Wakati Mwana-Kondoo alipotangaza Jambo hilo, akauvunja ule Muhuri, ndipo yule Mnyama mwingine. . . Unaona, hao wanyama wanashika zamu, juu ya kutangaza, “Njoo, uone.” Na Yohana, mahali alipokuwa amesimama, labda namna *hii*, anakuja hapa, wakati Mwana-Kondoo alipoifungua, na akaenda pale. Kwa kawaida. . .

254 Ngurumo inalia, kama tulivyoona katika Muhuri wa Kwanza. Naye anaangalia kuona jambo linalotukia. Naye anaona mtu akiya, kwanza, juu ya farasi mweupe. Anamwangukia akienda amepanda farasi. Na kuendelea mbele moja kwa moja, Yohana anamwona moja kwa moja hata mwisho. Yeye anamwona akishuka akienda, kwenye farasi wake mweupe, ana uta mkononi mwake, na nani—mpanda farasi anao, na hana mishale ya uta huo. Na jambo lingine analoona, anapata taji, anapanda moja kwa moja akienda zake.

255 Ndipo tunaona, basi, Mwana-Kondoo, huyu hapa anakuja tena, anafungua mwingine. Halafu anaangalia. Sasa hapa Yuaja fa—farasi mwekundu anakuja. Mtu huyu ana upanga mkononi mwake. Anaenda moja kwa moja akiwa amepanda farasi katika Maandiko, unaona, akiwa na upanga huu mkononi mwake, naye alikuwa aue na aondoe amani duniani.

256 Sasa Mwana-Kondoo anafungua Muhuri mwingine. Mwingine mmoja wa wale Wenye Uhai, kama mwanadamu, akasema, “Njoo, uone.” Sasa yeye anaenda pale, anaona hii ni nini. Na anapofanya hivyo, panatokea mpanda farasi juu ya farasi mweusi.

257 Sasa, jana usiku, tuliona ya kwamba mpanda farasi yule yule aliyempanda farasi mweupe alikuwa ndiye yule yule aliyempanda yule mwekundu.

258 Nayo ile Sauti ikasema, katikati ya wale Wenye Uhai, ikaita, unaona. Hapo, akaja kuona ilikuwa nini: Yeye alikuwa katika Wenye Uhai hawa. Naye akaona farasi huyu mweusi.

Na wakati . . . *kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na—na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru ma—mafuta wala divai.* (Unaona?)

259 Yule mpanda farasi, hebu na tumzungumze habari zake. Kama utamwalia yule mpanda farasi wa kwanza, kwamba yeye alikuwa ni nani. Nasi tuliona, usiku uliopita, Kimaandiko, ya kwamba yule mpanda farasi wa pili alikuwa ni mtu yule yule kabisa, ni kwamba tu alikuwa amepanda farasi mwingine. Ni nini kilitukia? Yeye alibadilisha huduma yake. Unaona? Sawa. Tuliona ya kwamba Yeye alikuwa mpinga-Kristo, naye alikuwa amebadilisha huduma yake.

260 Tuliona ya kwamba wakati yeye, kwanza, alikuwa tu ni farasi mweupe, akawa fundisho. Sasa, tumemrudisha kila mmoja wa hawa moja kwa moja kwenye Maandiko. Unaona?

261 Sasa, angalia mahali tulipo, usiku wa leo, ule wakati mwingine wa kanisa sasa. Unaona? Tunakuja kwenye wakati wa tatu wa kanisa sasa. Unaona? Tuko Katika wakati wa tatu wa kanisa barabara kabisa, ni sawasawa kabisa kama tu yule farasi wa tatu. Unaona?

262 Sasa, wakati wa kwanza wa kanisa, ulikuwa ni nini? Wanikolai walikuwa na fundisho, unaona, wa kwanza tu. Vema. Na basi, muda si muda tunajua, fundisho hili la Wanikolai, liliidhinishwa na likawa sawa, likaanza kutenda kazi. Nao wakamtia taji jamaa huyu. Ndipo, roho hii, mpinga-Kristo, ikafanyika mwili katika mtu fulani. Unaona? Nasi tunaona, baadaye, yeye anakuwa Ibilisi mwilini, pia; pepo anaondoka, na Ibilisi anaingia.

263 Na kama tu vile kanisa lile ni la namna hiyo, kanisa la mpinga-Kristo, linavyosonga mbele; vivyo hivyo Bibi-arusi amekuja na mambo mbalimbali: kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuendelea moja kwa moja, unaona, namna hiyo tu. Ila tu, wao walipata uamsho wao kwanza, nalo Kanisa linaupata wake mwisho. Miaka yao mitatu ya kwanza . . . hatua za kwanza tatu za hao waliopitia kwenye wakati wa giza; halafu ya tatu, hatua tatu, Kanisa linatoka; kutoka kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika Mungu aliyefanyika mwili akidhihirishwa kati yetu. Huyu hapa anakuja, kama mpinga-Kristo, kama nabii wa uongo, halafu mnyama, halafu katika wakati wa giza. Na kanisa linatoka katika wakati huo wa giza; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, Neno lililofanyika mwili, ndio njia sasa. Naye anashuka anaenda. Aha. Unaona jambo hilo? Yeye anashuka anaenda. Kanisa linapaa

juu. Unaona? Ni jambo kamilifu kabisa tu linavyoweza kuwa. Loo! linapendeza. Ninalipenda tu.

264 Mpanda farasi huyu ni yule yule, lakini hatua nyingine ya huduma yake.

265 Hatua ya kwanza, farasi mweupe, unaona, yeye alikuwa ni mwalimu tu, ni mwalimu mpinga-Kristo tu. Yeye alikuwa kinyume cha Neno la Mungu.

266 Na sasa unawezaje kuwa mpinga-Kristo? Mtu ye yote anayekana ya kwamba kila neno la hii si kweli, na kufundishwa vile vile lilivyo, ni mpinga-Kristo, ‘maana wao wanakana Ne—Ne—Ne—Neno. Naye ni Neno.

267 Sasa, hatua ya kwanza, farasi mweupe, yeye alikuwa ni mwalimu tu, lakini ni roho wa mpinga-Kristo katika mafundisho yake na tabia yake. Alikuwa hadhuru kitu. Hangedhuru kitu cho chote, ilivyoonekana; kuendelea tu. Hivyo ndivyo Shetani anavyoingia. Loo! yeye ni ndege mjanja.

268 Yeye alimwambia Hawa, akasema, “Sasa, unajua unatafuta maarifa. Wewe hujui mema wala mabaya.” Kasema, “Sasa, kama macho yako yangalikuwa yamefunguliwa, ungejua ni kitu gani.” Kisha kasema, “Tunda hilo ni tamu sana. Ni zuri. Lina—linapendeza macho. Ungelila sasa. Hujui kama ni zuri, ama si zuri, sivyo?”

“La, sijui. Lakini Mungu alisema tusifanye jambo hilo.”

“Lakini, loo! vema, najua, lakini . . .”

“Mungu alisema Yeye . . . tungekufa.”

269 Akasema, “Hakika Yeye hatafanya jambo hilo.” Unaona, tamu tu kama lilivyoeweza kuwa. Angalia kile lilichofanya.

270 Angalia roho hii ya mpinga-Kristo ikiinuka miongoni mwa kanisa la mwanzoni, fundisho la Wanikolai. *Nikao*, “kushinda” washiriki, kufanya mtu mtakatifu. Loo! ni kama tu ninii . . . “Vema, tunataka ushirika. Mbona, ninyi mmetawanyika hapa; hakuna mtu anayejijua alipo. Nadhani sote tunapaswa kuwa na madhehebu na tuwe tu watu tofauti. Unaona, tunaenda, tunaungana pamoja. Tunapaswa kuunda loji kutokana na jambo hili.” Na hivyo ndivyo ilivyo. Hakuna kitu kama Kanisa la Kikristo la Kimethodisti. Hilo si Kanisa; hilo ni loji. Batisti, hilo si Kanisa; ni loji.

271 Kuna Kanisa moja tu, na hilo ni Mwili wa siri wa Yesu Kristo. Nawe unazaliwa ndani ya Huo, hiyo ni kweli, kwa kuchaguliwa tangu zamani. Hiyo ni kweli. “Wote alionipa Baba watakuja. Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Mimi, watakuja Kwangu.” Kwa hiyo, hilo, jambo ndilo hilo. Yeye alininii tu . . .

272 Mwana-Kondoo anaketi pale, akifanya—akifanya upatanisho, mpaka wa mwisho atakapoingia. Ile kengele ndogo

inalia, Naye anatoka na kuchukua mali Yake basi, unaona, ni hayo tu; analileta kanisa Lake Nyumbani, raia Wake. Na anamtupa adui Wake katika Ziwa la Moto, na raia wake wote wanaingia mle pamoja naye, na ndiyo basi imekwisha. Ndipo tunatoka tunaingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu.

<sup>273</sup> Ni mpanda farasi yule yule, sasa. Hatua hii ya kwanza, yeye alikuwa hadhuru kitu. Na ya pili, sasa, kama mngalipanda juu kidogo, zaidi kidogo ya huyo; hatua ya pili, Biblia ilisema angepewa “taji.” Nao wakamtia taji, mtu, mtu mkuu. Unaona, wakamtia taji! Na, basi, Biblia haikumwita papa. Biblia ilimwita “nabii wa uongo.” Kwa nini? Ndiyo. Bila shaka, hana budi kuwa nabii wa uongo, kwa roho yake ya mpinga-Kristo, ambayo ilifundisha upinga-Kristo dhidi ya Neno la asili. Maana, kama yeye alifundisha dhidi ya Neno la asili, ilikuwa ni upinga-Kristo. Ilikuwa hivyo. Nalo Neno ni Mungu, unaona, Kristo. Vema. Sasa, baada ya jambo hilo, tunamwona yeye sasa ametiwa taji. Na wakati alipotiwa taji, sasa, yeye hana madhara kabisa na ni mnyonge. Yeye ni jamaa mdogo tu.

<sup>274</sup> Lakini basi katika lile Baraza la Nikea, yeye alitiwa taji, naye Konstatio akampa mali yote. Na ndipo alifanya nini? Ndipo yeye, unaona, Shetani, akampa kiti chake cha enzi na mamlaka. Biblia ilisema hivyo, kama tulivyopitia jambo hilo.

<sup>275</sup> Sasa, jambo lingine tunaloona, ya kwamba Ibilisi anatawala siasa zote ambazo zimekuwako ama zitakazokuwako baadaye. Tunaona jambo hilo katika Mathayo 4:11. Na sasa tunaona, basi, ya kwamba Shetani tayari alikuwa na siasa.

<sup>276</sup> Lakini yeye anajaribu kulipata Kanisa, kwa hiyo anashuka anaenda kulidanganya. Yeye anamchukua mtu wake mkuu, anamwingiza kwenye madhehebu fulani, na kumtia taji kama “halifa,” unaona, kristo fulani. Kristo alitenda kazi badala ya Mungu. Unaona, jamaa huyu ni halifa, badala ya Mungu. Unaona? Ni jambo lile lile hasa, “badala ya Mungu,” kile anachopaswa kuwa, halifa chini ya Kristo.

<sup>277</sup> Sasa, sasa, wakati alipofanya jambo hilo, ndipo yeye alifanya nini basi? Yeye, Shetani, alichukua nguvu zake za dini, ambazo tayari alikuwa nazo, kisha akachukua nguvu za kisiasa, ambapo tayari alikuwa ametiwa taji nazo, kisha akazikusanya pamoja.

<sup>278</sup> Ndipo baadaye akajifanyia taji nyingine juu ya kuzimu. Na hao walikuwa tayari wameaga dunia, kama wakilipa pesa za kutosha, yeye angewatoa humo. Unaona? Kwa hiyo sasa yeye ni ninii hii—yeye ni halifa juu ya Mbingu, juu ya pergatorio, kama yeye anavyotaka kupaita. Hakuna kitu kama hicho katika Biblia, unaona, lakini ilimbidi kufanyiza kitu fulani. Biblia ilisema hiyo imetokea kuzimu, na inarudi kule kule. Na, duniani, mtawala!

<sup>279</sup> Sasa yeye alipewa nini basi? Kwanza, yeye alikuwa na uta, bali hakuwa na mshale wo wote. Lakini sasa ana upanga

mkubwa mkononi mwake. Anaweza kufanya jambo fulani sasa. Ndipo anaruka kutoka kwenye farasi wake mweupe; yule farasi mweupe anaenda zake. Sasa yeye anapanda nini? Farasi mwekundu, damu, farasi mwekundu kama damu. Yeye anampanda huyo kwelikweli. Loo! hakika. Sasa yeye amepewa nguvu nyingi na upanga mkubwa, kuua, halafu yeye anaendesha farasi wake mwekundu kama damu.

<sup>280</sup> Tunaona, toka kwenye ule Muhuri wa Pili, uliovunjwa jana usiku, yeye alikuwa ameondoa amani duniani na watu waliuana. Na kwenye kitabu chake mwenyewe cha wafia imani, cha kanisa Katoliki la Roma, kinaonyesha ya kwamba wao waliwaua Waprotestanti milioni sitini na nane, tangu wakati wa Mtakatifu Hippo wa... baada ya Mtakatifu Agostino wa Hippo, mpaka mwaka wa elfu moja mia tano na themanini na kitu. "Milioni sitini na nane." Kitabu cha Schmucher kitiwacho *Great Reform*, kama ukitaka kukisoma, *Glorious Reform*, hasa, unaona. Sasa, milioni sitini na nane walionakiliwa kwenye kitabu cha wafia imani! Wakati mmoja wa watu wao wanaojiita watakatifu alipopata ufunuo ya kwamba mtu ye yote asiyekubaliana na kanisa la Kiroma anapaswa kufa kama mzushi, hilo basi liliwakusanya. Jamani, yeye alienda akimwaga damu! A—aliruka akampanda farasi wake mweupe... kwenye farasi wake mwekundu, akaenda zake amempanda. Loo!

<sup>281</sup> Sasa ile nguvu yake kuu inakuja. Yeye alifanywa halifa wa Mbinguni, na kuabudiwa kama Mungu. Mtawala wa dunia, kwa kuunganisha kanisa na taifa pamoja, ikamfanya kuwa mtawala duniani; hilo likampa taji. Yeye angeweza kuombea nafsi zitoke pergatorio. Pia angeombe... Alikuwa tu kama Mungu, duniani, badala ya Mungu. Pamoja na hayo, yeye alikuwa na nguvu kuu ya kumwua ye yote asiyekubaliana na amri yake. Ni nani atakayemwambia kitu? Kanisa haliwezi kusema kitu; yeye ndiye kiongozi wake. Taifa haliwezi kusema kitu; yeye ndiye kiongozi wake. Kwa hiyo, wao wakafa kwa mamilioni. Vijikanisa hivyo vyote, ndugu, vilivunjiliwa mbali, na kuuawa kinyama, na kulishwa kwa simba, na kila wazimu mwingine wo wote. Unaona? "Yule joka," Roma, "alimpa kiti chake na mamlaka." Biblia ilisema hivyo. Mnaona? Kwa hiyo yeye akampanda farasi wake wa kuigiza, farasi mwekundu, akienda kupitia kupitia katika damu za watu, mpaka akawa farasi mwekundu.

<sup>282</sup> Sasa Yohana anamwona amepanda farasi mweusi. Akabadilisha, kitu kingine.

<sup>283</sup> Sasa sina budi ku—kusema jambo hili jinsi vile tu lilivyoniya. Na basi na endapo liliinjia mimi nalo halikulingana na Maandiko mengine, basi Mungu kamwe hakulileta. Unaona, Maandiko hayana budi kuninii, kila moja, ni kitu kimoja tu kikubwa—kikubwa mno namna hiyo. Andiko halina budi kukubaliana na Andiko. Na lo lote ambalo ni kinyume cha

Maandiko . . . Kama huyo Malaika wa Bwana aliniambia jambo lo lote ambalo halikuwa ni Maandiko, nisingemwamini.

284 Nilisema, kule Chicago hivi majuzi, wakati mamia hayo yote ya wahudumu. . . Kuna mtu aliyekuwapo pale kwenye mkutano ule? Hakika. Mkutano ule Chicago, nilisema, “Sasa, nyote mnasema kwamba mna . . . Mlifikiri mngenipotosha hapa, juu ya jambo fulani.” Karibu kama ilivyo katika chumba hiki hapa sasa. Nikasema, “Ni kitu gani? Mna jambo gani dhidi yangu.” Nikasema, “Roho Mtakatifu alinionesha, masiku matatu yaliyopita, mahali ambapo kila mmoja wenu angekuwa. Nasi hatungekuwa kwenye hicho. . . Mwalizeni Carl hapa kama hilo si kweli.”

285 Na pale alikuwako Hank na hao wengine wote, “Hiyo ni kweli.” Nyote mlikuwako kule kusikiliza.

286 Nikasema, “Sasa mnanipinga mimi, juu ya Mafundisho yangu. Hiyo ndiyo hoja yenyewe. Sasa nataka mmoja wenu aje hapa, na achukue Biblia yake aisimame karibu nami, na ayakanushe.” Lilikuwa kundi nyamavu sana mtu ulilopata kusikia. Nikasema, “Mna shida gani?” Nikasema, “Basi, kama mnajua hamwezi kulipinga Neno, basi ondokeni mgongoni kwangu. Ninyi Madaktari wa Uungu na kadhalika, na mnazungumzia vile, mnajitambulisha wenyewe kama ‘Daktari,’ ‘Daktari,’ ‘Daktari.’ Nami ni ninii. . .” (Loo! mimi na Ndugu Woods tunasema, “cheechaka,” ama, “mbumbumbu.”) “Sina elimu, sijawahi kupitia seminari yo yote ama shule. Lakini chukua Biblia yako na uje hapa na usimame karibu yangu, kanusha uzao wa nyoka, ubatizo katika Jina la Yesu, ama yo yote ya mambo hayo ninayofundisha.” Hakuna mtu aliyesema neno. Nyote mnajua jambo hilo. Hilo lilikuwa ndilo kundi lililo nyamavu sana ulilopata kuona.

287 Mnaona, wao wanajivuna sijui kama kitu gani. Sasa, basi kitu chenyewe ndicho hiki hapa. Mimi siamini katika kubishana na watu, isipokuwa inapofikia mahali ambapo wanajaribu kukukokota kukuingiza katika jambo hilo. Nami nisingalienda, lakini Roho Mtakatifu aliniambia, akasema, “Nenda kule. Nitakutetea.”

288 Nikawaambia, siku tatu ama nne kabla ya wakati. Nyote mlikuwako kule mkamsikia Bw. Carlson na hao wengine, na—na Tommy Hicks. Na hao wote wanaoketi hapo. Ndipo nikaenda, siku tatu kabla, basi nikasema, “Itawabidi kupabatilisha mahali hapo.”

289 Ulikuwa ni usiku wa mvua kubwa. Nilikuwa na mkutano. Yeye akasema, “Nenda, usimame kwenye lile dirisha, kwenye ule mlango wa tatu pale.” Nami nikaenda pale na kusimama. Nikaangalia nje namna hiyo.

290 Akasema, “Wao wamekutegea mtego. Watakuomba uzungumze kwenye Shirika la Wahudumu wa Chicago ya Juu.”

Kasema, “Wamekutegea mtego, juu ya mafundisho yako ya Neno Langu.”

<sup>291</sup> Akasema, “Sasa, wao watabatilisha mahali pale kule. Hawatapapata. Nao watapata mahali, ambapo ni pa hudhurungi.” Kasema, “Ni pa namna hii.” Nikasimama, nami nikajiona niko penye kona; nikaangalia kule nyuma nami nikaona. Nikawaona wote pale. Nikawaona hao wahudumu wote wameketi pale, jinsi walivyokuwa wameketi. Nikawaangalia wote kila mahali. Naye akasema . . .

<sup>292</sup> “Loo!” nikawaza, “Afadhali nisiende kule basi, Bwana, kama watafanya jambo hilo. Sitaki kuwaudhi wala kufanya jambo lo lote baya.”

Yeye akasema, “Nenda. Nitakutetea.” Alinitetea. Hiyo ni kweli.

<sup>293</sup> Sasa, ninyi nyote, kuna mashahidi papa hapa, walikuwa wameketi papo hapo na wanajua jambo hilo ni kweli. Hiyo ni kweli. Vema, mna hizo kanda hapa, pia. Lakini, haya basi, unaona.

<sup>294</sup> Sasa, sasa hii hapa siri ya jambo hili. Na sasa, Hiyo, wakati Yenyewe iliponifunulia kwangu alfajiri na mapema leo, kabla hakujapambazuka. Ndipo nikaenda upesi kwenye Maandiko na kuanza kuangalia, kulichunguza. Hiyo hapo. Mitatu kati ya Hiyo, kufikia wakati huu, imefunuliwa dhahiri kimbinguni. Naam. Sasa hii hapa siri ya yule farasi mweusi, kulingana na vile ilivyofunuliwa kwangu.

<sup>295</sup> Yeye alianza kumpanda katika wakati wa nyakati za giza. Hilo ndilo farasi mweusi alilowakilisha, zile nyakati za giza, kwa maana ilikuwa ni wakati wa usiku wa manane kwa waamini wa kweli waliosalia. Angalieni sasa katika wakati ule wa kanisa, wakati huo wa katikati wa kanisa, wakati wa giza wa kanisa. Angalia jinsi Yeye anavyosema, “Una nguvu kidogo tu.” Ilikuwa ni usiku wa manane kwao, kwa mwamini wa kweli. Sasa angalia. Karibu kila tumaini lilikuwa limeondolewa kwenye Kanisa la kweli, kwa maana jamaa huyu alitawala kanisa na taifa pia. Watafanya nini? Unaona, Ukatoliki ulikuwa umetawala, kanisa na taifa pia. Na wote, ambao hawakubaliana na Ukatoliki, waliuawa. Hiyo ndiyo sababu alikuwa amepanda farasi mweusi. Basi angalia jinsi alivyotenda jambo ovu, unaona, ndipo unaweza kuona. Nawe ninii tu . . . Kama unajua historia yako, iangalie, ndipo utaninii . . . Vema, hata haitakubidi kuijua, ku—kujua jambo Hili. Sasa angalia. Tumaini lote lilikuwa limekwisha. Huyu ndiye yule farasi wake mweusi.

Sasa, yeye alimpanda farasi wake mweupe, ujanja.

<sup>296</sup> Kisha akapewa mamlaka; akaondoa amani, akaua mamilioni. Hivyo ndivyo alivyokuwa anataka kwenda kufanya alipompanda akienda zake. Na angali anafanya jambo hilo. Unaona?



<sup>297</sup> Sasa, huyu hapa yuko juu ya farasi wake mweusi sasa, akijitokeza. Wakati wa giza, huo ulikuwa ndio wakati ule. Mnamo wakati tu baada ya kanisa kuimarika, na likapata mamlaka, walinyamazisha kila kitu kinginecho. Na likasafiri moja kwa moja, yapata, mamia na mamia na mamia ya miaka, ndiyo kila msomaji anayojua kama nyakati za giza. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ndio, zile nyakati za giza. Huyu hapo farasi wako mweusi, akiwakilisha wakati ule wa giza. Sasa, matumaini yote yalikuwa yamekwisha; hakuna tumaini lo lote. Kila kitu kilionekana ni giza, kwa maskini wale waamini wachache. Sasa, hiyo ndiyo sababu unaitwa, uliwakilishwa, na farasi mweusi.

<sup>298</sup> “Mizani zake, ama mizani zake, mkononi mwake,” unaona. Akipaza sauti, “Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vipimo vitatu vya shayiri kwa nusu rupia.” Unaona, kwa kweli, hiyo ni kusema, ngano na shayiri ni vitu vya maisha ya kawaida. Hivyo ndivyo vinavyotengeneza mkate na kadhalika. Lakini, unaona, yeye alikuwa akitoza pesa kwa ajili ya vitu hivi. Maana yake, ni kwamba, yeye alikuwa akiwatoza pesa raia wake kwa ajili ya tumaini la maisha alilokuwa anawapelekea, kwa kufanya. . . Yeye alianzia katika wakati uo huo, wa kuwafanya walipie maombi, akiwatoza pesa kwa ajili ya maombi. Wangali wanafanya jambo hilo; maombi ya siku tisa mfululizo.

<sup>299</sup> Maana, yeye alikuwa anafanya nini? Akichukua utajiri wa ulimwengu. Ile mizani, akipima, “Kibaba cha ngano kwa nusu rupia; vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia.” Yule mpanda farasi aliyempanda farasi mweusi, unaona, yeye alikuwa akifanya. . . akiwanyang’anya raia wake pesa zao. Wakati, Biblia inabashiri ya kwamba yeye anashikilia, karibu, utajiri wote wa ulimwengu. Kama tulivyosema jana usiku juu ya Urusi, na yote hayo, ya kwamba wao wanachukua pesa zote tu na kuwanyang’anya watu tu kila walichokuwa nacho, kila kitu. Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo.

<sup>300</sup> Sasa angalia. Unaona mahali ambapo kule kujipatia pesa kwa siku nyingi, kutoka kanisani, kulikoanzia? Ukimbieni upuuzi huo; kuunda madhehebu, kitu fulani kikubwa, dola milioni hapa. Basi—basi mnaona mama yake ni nani?

<sup>301</sup> Asante, Bwana. Loo! jamani! nina furaha sana. Naam, bwana. Vema. Imekuwa ni neema Yake. Basi. Vema. Vema.

<sup>302</sup> Ulikuwa ni wakati wa usiku wa manane. Je! mnaelewa hilo sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na hapa anatoza fedha kwa maisha ya namna hiyo, hiyo ndiyo shayiri yake na takataka nyingine, vitu vya kawaida; havikuwa vya kiroho, sasa. Ilikuwa ni shayiri, unaona, kwa hiyo, na mkate wa shayiri na mkate wa ngano. Yeye alikuwa akilipisha maisha ya namna hiyo aliyokuwa anawapa raia wake. Akilipisha kwa ajili ya maombi yaliyotolewa na makasisi, kuwaomba watu watoke pergatorio.

Kutoza pesa! Sasa ninatoa jambo hili moja kwa moja kutoka kwenye historia. Akilipisha, nadhani, ni maombi ya siku tisa mfululizo, nafikiri, kila mtu anajua ni nini. Maombi ya siku tisa mfululizo, nafikiri hilo ni jambo unalopaswa kufanya, unajua, kitubio fulani. Mtu fulani hana budi kuuza hilo. Kujiletea mali ya ulimwengu kwake, mwenyewe, katika kanisa lenyewe. Naye angali anampanda. Loo, hakika anampanda. Naam, bwana. Angali amepanda farasi!

<sup>303</sup> Angalia. Hii hapa sehemu nzuri sasa. Angalia.

. . . *wala usiadhuru* divai hii na mafuta.

<sup>304</sup> “Ni kidogo tu kilichobakia pale, lakini usikiguse Hicho!”

<sup>305</sup> Sasa, mafuta ni. . . yanawakilisha Roho, Roho Mtakatifu. Nitawapa vifungu vichache mkitaka. Kuna Maandiko mawili. Katika Mambo ya Walawi, 8:12, ambapo Haruni, kabla hajaingia, ilimbidi kutiwa mafuta, mnajua. Na katika Zekaria 4:12, juu ya mafuta kuja, yakimiminika kupitia katika mabomba, kisha akasema, “Hii ni Roho Yangu, Mafuta.” Jambo lingine, kama ukitaka kuona Mathayo, 14. . . 25, kulikuwako na mwanamwali mjinga, ama 25:3, yule mwanamwali mjinga hakuwa na Mafuta, hana Roho. Na Mathayo 25:4, yule mwanamwali mwerevu alikuwa na Mafuta kwenye taa yake, amejazwa Roho. Roho! Mafuta ni mfano wa Roho. Loo! utukufu! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Vema. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Vema. Sasa, mafuta yanawakilisha Roho.

<sup>306</sup> Na divai inawakilisha changamko la ufunuo. Loo! ka—karibu nikimbie huku na huko kila mahali. Nashangaa sikuwaamsha majirani, wakati Bwana aliponionyesha jambo hilo, unaona, “changamko la ufunuo.” Unaona?

<sup>307</sup> Mafuta na divai, katika Biblia, vinahusiana pamoja, sikuzote. Nilichukua itifaki na kuangalia. Kuna mlolongo wa hayo, hiyo—namna *hiyo*, ambapo divai na mafuta vinaambatana, sikuzote. Unaona?

<sup>308</sup> Wakati Kweli ya Neno la Mungu lililoahidiwa imefunuliwa kwa kweli kwa watakatifu Wake ambao wamejazwa na Mafuta, wote wanachangamka. Divai ni mchangamko. Utukufu! Ninalihisi hivi sasa kabisa. Kuchangamshwa na furaha, vifijo! Unaona? Na, inapofanyika hivyo, ina matokeo yale yale kwao ambayo—ambayo divai huwa nayo kwa mtu wa kawaida. Kwa sababu, wakati ufunuo umetolewa, wa kweli ya Mungu, na mwamini wa kweli aliyejazwa na Mafuta, na ufunuo unafunuliwa, kuchangamka kunakuwa kuuu mno mpaka Yeye anamfanya kutenda isivyo kawaida. Kweli. Utukufu! [Kusanyiko linafurahi—Mh.] Unaona, hicho ndicho kinachowatukia basi. Hii ni kweli, kunawamfanya watende isivyo kawaida.

<sup>309</sup> Sasa, kama ukitaka Maandiko kwa ajili ya jambo hili, anza tu kusoma Matendo 2. Wako wapi? Wao walikuwa na ahadi

waliyokuwa wamepewa. Wakati ahadi yote ya Roho Mtakatifu ilipomwagwa juu yao. Na ilikuwa . . . Ilihibitishwa Kimaandiko. Sasa, unaona, ninii . . .

310 Vipi kama wao wangelisema . . . “Sasa, ngoja, Yeye alitwambia tungojee hapa kwa ajili ya huduma yetu.” Na baada ya siku nane, huenda wangesema, “Vema, nitawaambia, enyi vijana,” Marko akamwambia Mathayo, “Ni—ninaamini tayari tumempata, jamani. Sivyo? Mnaona, tumempata tayari. Wakati tunapongojea huduma yetu sasa, inatupasa tuondoke twende zetu, tukihubiri. Yeye alitwambia tuje hapa na tungojee, na hizi ni siku nane tumekuwapo hapa.”

“Vema, na tungojee nyingine.”

311 Siku tisa zikafika. Ndipo Marko akaja, ama—ama—ama labda mmoja wa hao wengine, Yohana, akasema, “Ni—ni—ninaamini haitupasi kungojea zaidi tena. Ninaamini tumempata tayari. Sivyo?”

312 Ndipo ninaweza kumwona Simoni, maana yeye alikuwa na funguo, unajua. “Sasa ngojeni kidogo, enyi vijana! Maandiko yana kitu fulani cha kusema juu ya jambo hili. Yeye hakutuambia kamwe tungojee siku ngapi zaidi. Yeye alisema, ‘Ninyi kaeni hapo hata! Kaeni hapo hata unabii wa Yoeli utakapotimia, hata unabii wa Isaya utakapothibitishwa.’”

313 “Kwa maana kwa vinywa vya kugugumiza na kwa lugha ngeni nitanena na watu hawa. Na huku ndiko kuburudika.” Hii ndiyo divai inayomwagwa. Divai ni nini, katika Biblia? Viburudisho. “Hiki ndicho kiburudisho kinachotoka katika Uwepo wa Bwana.” Mnaona? Halina—halina budi kuwa ni la Kimaandiko sasa. Unaona?

314 Kwa hiyo, unaona, divai inawakilisha changamko la ufunuo. Na wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, nao wakauona Moto wa Mungu ukiwashukia, jamani, hilo lilianza kuwachangamsha. Na muda si muda wajua, walichangamka mno hata watu kwa kweli wakafikiri walikuwa wamelewa, lakini wao walikuwa wamechangamshwa na ufunuo. Kwa ninii ya Mungu . . . Huu hapa! Ufunuo wa Mungu uliohibitishwa, ukifanywa dhahiri kwao, walifurahishwa Nao. Mungu aliahidi jambo hilo. Hapa lilifunuliwa kwao, na kuthibitishwa kwao. Amina! Hapa palikuwapo na mtu amesimama pale, akisema, “Jambo hili ndilo Lile! Jambo hili ndilo Lenyewe!” Na hilo hapo, likithibitishwa kwa ishara ile ile tuliyo nayo leo. Hilo—hilo hapo changamko kwa kufunuliwa. Unaona? Na, sasa, kwa kweli walikuwa nao wakati huo.

315 Hiyo ndiyo sababu Petro aliweza kutoka huko nje, na kusema, “Mbona, enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu, nisikilizeni mimi. Ninyi Madaktari wote wa Uungu, sikilizeni yale nitakayowaambia, mnaona.”

<sup>316</sup> Loo! ni ajabu jinsi gani! Kufunuliwa! Kufunuliwa! Walichangamka sana walipoliona limethibitishwa. Huo daima hufanya hivyo tu. Daima hufanya hivyo.

<sup>317</sup> Wakati nikiona kwamba Mungu aliahidi kufanya jambo fulani katika siku hii, wakati Yeye aliahidi kuvunja Mihuri hii katika siku hii ya mwisho! Na hamjui hiyo furaha, huo utukufu, wakati nilipomwona Yeye akifunua jambo hili, nikisimama pale na kuliona likitukia! Na kujua ya kwamba nitamchukua mtu ye yote, kumwamuru: Yeye kamwe hajawahi kutuambia jambo moja ila lilitukia vile vile. Halafu kuona furaha iliyoyoni mwangu, ninapona ahadi yake kwa ajili ya siku hizi za mwisho, kama alivyoahidi kufanya. Na hapa ninaliona limethibitishwa na kufanywa kamilifu sana. Mimi ni ninii tu... Mnanisikia nikisema, "Ninajisikia mwana dini." Sababu yake ni hiyo. Lile changamko ni kubwa sana, karibu ni—ni—niko tu—tu kuanza kukatika vipandevipande, unajua. Changamko, kutokana na ufunuo! Vema.

<sup>318</sup> Wao walichangamka sana, kwa u—ufunuo, hata wao walithibitisha, vema, ile ahadi. Sasa, loo! jamani! Hapo ilitokea furaha ya kuchangamka, mpaka watu wakasema, "Wamelewa kwa mvinyo mpya," wakati Mungu alipofunua ahadi Yake kwao. Na si kwamba tu Yeye aliifunua, bali aliithibitisha.

<sup>319</sup> Hivyo ndivyo nilivyosema daima. Mtu anaweza kusema jambo lo lote, naam, yeye angeweza tu kuwa hodari kusema lo lote; lakini wakati Mungu anapokuja na kuthibitisha jambo hilo!

<sup>320</sup> Sasa, Biblia ilisema, "Kama kuna mtu mmoja kati yenu, anayedai kwamba ni wa kiroho au ni nabii, kama akisema mambo haya na yasitimie, basi msimjali. Msimwogope, hata kidogo. Msimwogope mtu huyo. Lakini akilisema na litimie; huyo ni Mimi, unaona. Mimi, Mimi niko katika jambo hilo. Hilo linathibitisha kwamba ni Mimi vipi."

<sup>321</sup> Na, halafu, maskini yule mwanamke Msamaria. Wakati Maandiko yaliposema ya kwamba Masihi huyu angetenda mambo haya, Naye huyu hapa amesimama na kutimiza sawasawa yale Maandiko yaliyosema. Yule mwanamke akasema, "Huyo hapo. Njoni, mmwone Mtu! Je! hilo silo jambo lile hasa ambalo Maandiko yalisema lingetendeka?" Unaona, yeye alichangamshwa na ufunuo. Ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Alichangamshwa na ufunuo, hapo ulipothibitishwa. Unaona? Hiyo ni kweli. Yeye alijua ya kwamba kulikuwako...

<sup>322</sup> "Tunajua ya kwamba Masihi yuaja, aitwaye Kristo. Na atakapokuja, atafanya mambo haya." Yeye aliona.

Ndipo akasema, "Mimi Ndiye."

<sup>323</sup> Ndipo changamko likaanza. Naye huyoo akaenda zake, akipaza sauti na akashuka mjini. Aliacha mtungi wake wa kale

wa maji, na akashuka akaenda kule, na kuwaambia wale watu, “Njoni, mwone!”

324 Sasa, kama mngalijua desturi za Mashariki, hilo ni kosa kwake kufanya hivyo. Naam, bwana. Mwanamke wa namna hiyo, hakuna mtu angelimsikiliza. La, bwana. Unaona, yeye alikuwa na alama, na wakati yeye. . . Kama angalienda zake barabarani namna hiyo, na kufanya hivyo, wanaume barabarani hawangemjali.

325 Lakini, ndugu, yeye alikuwa na Neno la Uzima pale! Alikuwa amechangamshwa. Ungeweza. . . Ilikuwa ni kama kujaribu kuzima nyumba, inayungua moto, katika siku yenye upepo. Loo, kuna kitu kinachoupulizia! Yeye alikuwa—alikuwa tayari. Naam, wao hawakuweza kuuzima Huo. Huo ulikuwa ni Moto wa Mungu unaowaka. Ndio, bwana. Akasema, “Kama hamwamini hilo ni kweli, hebu njoni tu hapa mahali ambapo mkutano unaendelea. Nitawaonyesheni kitu hicho.” Naam. Hivyo ndivyo ilivyo. Naam. Ndio, bwana.

326 Na kwa hiyo hao watu wakaenda kule. Naye hakufanya jambo hilo mara moja zaidi. Lakini wao walijua jambo fulani lilikuwa limetukia kwa mwanamke huyo. Yeye alikuwa amebadilika, kwa hiyo wao walimwamini. Naam, bwana. Walimwamini.

327 Maana, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia ahadi ya Mungu, Neno la Mungu, na kuliona likifanywa dhahiri.” Maana, Hilo ni mbegu. Na wakati linapopandwa, litakuwa Hai. Litazaa kile tu linachonena habari zake. Kama halizai, basi si Mbegu ya Mungu. Ama, mpanzi hakujua jinsi ya kulipanda; hakutumwa na Mungu, kupanda Mbegu. Huenda anazipanda juu ya mwamba ama kitu fulani. Unaona? Kwa hiyo una—kwa hiyo unaona, mpanzi akipanda Mbegu, Mungu huishughulikia, inaangukia mahali pazuri, unaona. Loo! jamani!

328 Ndipo linamwambia nini huyu mpanda farasi mweusi? Usidhuru divai Yangu na Mafuta Yangu! Usiviguse, divai Yangu na Mafuta! Nimesaliwa na kidogo tu kule, lakini kungali kuna kidogo kule. Naam. Sasa unaweza kwenda zako na kupima maisha ya namna hiyo unayotoa; hiyo ni juu yako. Utaenda kulipia hayo mbele ya safari. Lakini ukikutana na divai hiyo na Mafuta hayo, usiguse!” Loo! jamani! Kama unaweza, kama u- . . .

329 Kwa maneno mengine, ni kama hivi, “Kama ukishika baadhi ya wana Kondoo Zangu, waliojazwa na Mafuta Yangu na divai, unaona, divai na Mafuta ya Neno lililo safi, unaona, nawe unaenda kuwaua. Maana, wewe, unafanya hivyo. Hivyo ndivyo unavyofanya. Usiwalazimishe kusema ‘Salamu Mariamu,’ ama kufanya jambo kama hilo, ama baadhi ya kanuni zako za imani. Usiwaguse. Wao wanajua wanakoenda, kwa maana wametiwa Mafuta Yangu. Na kwa kutiwa kwa Mafuta Yangu,

wao wana divai ya furaha, maana wanajua Neno Langu la ahadi, 'Nitawafufua tena.' Usidhuru Hao! Usiende ukajaribu kuwachafua. Maana, usiwakaribie hata kidogo. La." Wote . . .

330 Yeye hulithibitisha Neno Lake na kulingiza. Wao walijua. Walijua watafufuka tena. Loo! jinsi ninavyopenda jambo hilo! Whiu! Wao watafufuka tena. Huyu hapa farasi mweusi anakuja, akiendeshwa sasa, nyakati za giza.

331 Palitokea farasi mweupe; tuliona alilofanya, kikamilifu. Huyu hapa farasi mwekundu anakuja; tunaona alilofanya hasa. Huyu hapa farasi mweusi anakuja. Unaona, ni mpanda farasi yule yule wakati wote, analofanya, moja kwa katika nyakati zote.

332 Sasa tunaona, yeye aliipima na kuilipisha, kweli kabisa: ngano, ya kawaida, maisha ya kawaida. Hiyo ndiyo waliyokuwa wanatumia.

333 Lakini, ikimwakilisha; Roho, Mafuta; na furaha ya divai. "Hayo Maisha ya kiroho, usiyadhuru Hayo. Yaache!" kwa maneno mengine, "Ewe Roma, usiyaguse Hayo! Ni Yangu! Hayo ni Yangu!"

334 Sasa nina jambo lingine hapa ninalotaka mjue. Angalia, haikuwa mmoja wa wale Wenye Uhai wanne ambaye alisema, "Usiyadhuru Mafuta na divai." Uliliona jambo hilo? Wale Wenye Uhai wanne walikuwa wakizungumza, lakini . . . Angalia, hebu nisome hapa, kidogo tu, unaona, sasa.

. . . *kibaba*, nusu rupia, *kwa—kwa nu—*. . . *ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru divai na . . . mafuta.*

335 Sasa sikiliza hapa.

*Ni—nikasikia sauti katikati ya wenye uhai wanne, . . .*

336 Ilikuwa ni nini? Mwana-Kondoo! Amina! Haikuwa ni wale Wenye Uhai wanne. Mwana-Kondoo ndiye aliyesema jambo hilo. Kwa nini? Yeye anaenda kuchukua walio Wake. Hao ni Wake. Amewakomboa. Unaona? Amina! "Usiyaguse hayo Mafuta!" La, bwana. Si wale Wenye Uhai wanne, lakini Mwana-Kondoo Ndiye aliyesema jambo hilo. Na, loo! jamani! Mwana-Kondoo! Si . . . Wale Wenye Uhai wanne hawakutangaza jambo hili. Mwana-Kondoo alilisema, Yeye Mwenyewe.

337 Wakati wale Wenye Uhai wanne waliposema, "Njoo uone," nao wakaenda, nao wakaliona namna hiyo.

338 Naye akasema, "Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na kwa kiba-. . . na kiasi fulani namna *hii*, na kiasi fulani cha shayiri." Lakini basi Mwana-Kondoo akapaaza, moja kwa moja kati yao, akasema, "Wala usiidhuru divai na Mafuta!" A-ha. Hiyo ni kweli. Loo! jamani! Sikilizeni hilo, "Usiyadhuru Hayo, loo! la sivyo utayajutia siku moja." Loo! jamani!

Saa tatu na nusu.

<sup>339</sup> Vema, ninavyofahamu mimi kwa uwezo wangu wote, na nijuavyo mimi kabisa, na kwa yote ninayoamini moyoni mwangu, hiyo ndiyo maana halisi ya hiyo Mihuri mitatu. Ninataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya hilo. Nami nitasema jambo hili, ya kwamba, ndio ufunuo alionipa Yeye. Yeye alinipa huo, ufunuo Wake. Nami ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho.

<sup>340</sup> Kesho usiku tutamchukua huyo mpanda farasi wa kijivu. Na sasa sijui. Sijui. Mungu anajua ya kwamba jambo hilo ni kweli. Sijui neno hata moja juu yake. La.

<sup>341</sup> Niliangalia kwenye maandishi yangu ya zamani niliyokuwa nayo miaka mingi iliyopita. Nilimwona Ndugu Graham Snelling muda mchache uliopita; huenda ametoka. Lakini, ninakumbuka wakati nilipokuwa nikihubiri hapa, hapo nyuma. Nilichunguza nione niliyosema miaka mingi iliyopita. Siku moja nilikuwa nikipitia Kitabu cha Ufunuo, niliwachukua hao wapanda farasi wanne wakati mmoja.

<sup>342</sup> Nikasema, “Farasi mweupe, huyo alikuwa ni lile kanisa la mwanzoni, hapana shaka.” Nilisoma hayo kutoka kwenye kitabu cha Wasabato. Nami nilisoma jambo fulani mle. Nikasema, “Hilo lilikuwa ni lile kanisa la mwanzoni lililotoka likaenda, likishinda.” Na aliyefuata alikuwa ni farasi mweusi, nikasema . . . Sikumbuki sasa vile niliyomwita huyo farasi mweusi. Nilisema . . .

<sup>343</sup> Ama, “Yule farasi mwekundu,” namaaanisha, nilisema, “farasi huyo labda alimaanisha ya kwamba—ya kwamba shida inakuja, na ina maana kwamba vita vingi vitapiganwa, ama kitu kama hicho.” Nikasema, “Labda kutakuwa na vita vingi.” Nikasema, “Hilo ndilo litakalotokea.” Kisha nikasema, “Yule—yule farasi wa kiji- . . .”

<sup>344</sup> Ama, “Fa—farasi mweusi,” nikasema, “huyo—huyo anamaanisha ya kwamba—ya kwamba labda kutakuja wakati wa giza duniani, wakati nyota zote zita—zitaataa kuwaka; jua litatua, wala mwezi hautatoa mwangaza wake.” Nikasema, “Hiyo labda ndiyo maana yake.”

<sup>345</sup> Nikasema, “Yule farasi wa kijivujivu, anamaanisha magonjwa mengi yanakuja.” Sasa, sijui maana yake. Lakini, hiyo, hiyo ndiyo iliyokuwa tafsiri yangu wakati huo, ‘maana nililichukua tu kwa uwezo wangu wote nilivyoweza, nikiwa nimesimama hapa mimbarani.

<sup>346</sup> Lakini, loo! karibu nimesema jambo fulani! Vema. A-ha! Loo! Mta—mtaona. Angalienu tu, unaona.

<sup>347</sup> Sasa, jamani, hivi hatuna furaha kwa ajili ya saa hii tunayoishi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tunapoona mambo haya yote yakifikia kileleni, ninafikiria:

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,  
Ishara walizotabiri manabii;  
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa  
na hofu;  
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

Siku ya ukombozi imekaribia,  
Mioyo ya watu inazimia kwa uoga;  
Jazweni Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni  
safi,  
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!  
(Loo! jamani!)

Manabii wa uongo wanasema uongo,  
wanaikana Kweli ya Mungu,  
Ya kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu  
wetu;

Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Lakini tutatembea mahali walipokanyaga  
mitume.

Kwa kuwa siku ya ukombozi imekaribia,  
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;  
Jazweni Roho, taa zenu ziwe zimetengenezwa  
na ni safi,  
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

<sup>348</sup> Hilo si ni la ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]  
Ninapenda hilo. Ukombozi umekaribia.

Na itakuwa Nuru wakati wa jioni,  
Njia ya Utukufu kweli mtaiona;  
Katika njia ya maji, ndiko kwenye Nuru leo;  
Ukizikwa katika Jina la thamani la Yesu.  
Watoto kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,  
Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani;  
Nuru ya jioni imekuja,  
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

Yeye ni Neno! Loo! jamani! Ajabu sana!

Karibuni Mwana-Kondoo atamchukua Bibi-  
arusi Wake awe karibu Naye daima,  
Jeshi lote la Mbinguni litakutanika;  
Loo! itakuwa ni tamasha lenye utukufu,  
watakatifu wote wamevaa mavazi meupe  
yasiyo na doa;  
Nao pamoja na Yesu watasherehekea Milele.

Loo! “Njoo ule,” Bwana aita, “Njoo ule;”  
Loo!, unaweza kula meza ya Yesu daima;  
Yeye aliyeulisha umati wa watu, akageuza maji  
yakawa divai,  
Wenye njaa sasa anawaita, “Njoni mle.”



Loo! “Njoo ule,” Bwana aita, “Njoo ule;” (Ule Neno!)

Unaweza kula kwenye meza ya Yesu daima;  
Yeye aliyeulisha umati wa watu, akageuza maji  
yakawa divai,

Wenye njaa sasa anawaita, “Njoni mle.”

349 Loo! jamani! Mna njaa? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]  
“Heri wenye njaa na kiu ya haki.”

350 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]  
Mnampenda? Sauti ya *Nampenda*, unajua. Hebu sote na  
tusimame sasa, na tuinue mikono yetu na kumwabudu Yeye.  
“Nampenda, nampenda kwa sababu Yeye alinipenda kwanza.”  
Vema, sote pamoja sasa.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

351 [Ndugu fulani ananena kwa lugha. Ndugu Branham  
anatulia—Mh.] Iweni wenye uchaji sana. Tuna mfasiri hapa,  
Ndugu Higginbotham. Sijui kama yeye yuko hapa usiku wa leo,  
ama hayuko. Tunataka kujua aliyotwambia. Ngojeni kidogo tu.  
Hapa, hapa . . . [Dada anafasiri.]

352 Hakika, Bwana asifiwe! Imani yangu imeinuliwa juu katika  
Mungu. Ninyi, ninyi, mnampenda Yeye, usiku wa leo, kwa  
moyo wenu wote? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Loo! msifuni,  
na msemi, “Asante, Bwana Yesu!” [Kusanyiko linamtukuza  
Mungu.]

353 Jinsi tunavyokupa sifa, kwa mioyo yetu yote, Bwana! Mungu  
apewe utukufu!

354 Hebu mtukuzeni, enyi watu wote. Mungu awe pamoja  
nanyi. [Kusanyiko linaendelea kufurahi na kumtukuza Mungu—  
Mh.]



*UFUNUO WA MIHURI SABA*  
(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Machi mpaka tarehe 24 Machi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Machi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)